Jumanne Septemba 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581802

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**ARTETA AANIKA SPURS ILIVYOMNYIMA USINGIZI** UK. 21

# BAKWATA: Utekaji na mauaji vichunguzwe na tume huru

• **Majaliwa:** Tunafanyia kazi, ila kuna chokochoko... *Ukurasa 2*

UKURASA WA 4



**Wakulima** tumbaku walia kulazimishwa kutia saini mikataba ya uuzaji mazao yao

UKURASA WA 4



**Utata** wakala wa fedha kutoweka akifuatilia madeni yake ya kibiashara

UKURASA WA 10



**Wahofia** kupata saratani, TB kisa magari ya zebaki kuoshwa jirani na makazi yao



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakary Zubeir Bin Ally wakati wa Baraza la Maulid Kitaifa lililofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu, Geita jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## ACT: Vigogo wamefyeka mikoko Dar na kujenga ufukweni

UKURASA 3

## CRDB yaja na mradi wa bil. 790/-, umeme vijijini, ajira 500 mgodini

UKURASA 8

**MICHEZO** **FADLU AIONA SIMBA TOFAUTI KWA MKAPA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# BAKWATA yataka Tume Huru kuchunguza utekaji na mauaji

**Na Alphonse Kabilondo,**
GEITA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika Baraza la Maulid Kitaifa lililofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu, Geita jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

BARAZA la Waislamu Tanzania (BAKWATA) limeshauri serikali kuunda tume huru kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa matukio ya watu kutekwa na kuawa yanayoripotiwa nchini.

Kukiwa na rai hiyo ya BAKWATA, Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa amesema serikali inafanyia kazi changamoto hiyo ya kiusalama, akidokeza kuwa "kuna baadhi wameanza kuleta chokochoko katika taifa".

Rai ya kuundwa tume huru ya uchunguzi wa matukio ya utekaji na mauaji nchini ilitolewa jana na Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaj Nuhu Mruma, wakati wa maadhimisho ya Baraza la Maulid yaliyofanyika kitaifa mkoani Geita kwenye Viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu.

Alisema Baraza hilo linaendelea na litaendelea kupinga matukio ya ukatili na utekaji kwa kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kuthaminiwa utu wake.

"Tume hiyo itakapoundwa ikatende haki kwa kuzingatia sheria. Kwa kuwa huu ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwakani Uchaguzi Mkuu, ni vyema ukafanyika kwa uhuru na haki," alisema.

Alhaj Mruma pia alitoa wito kwa Waislamu na Watanzania kwa ujumla kujitokeza kushiriki katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura pamoja na kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kiongozi huyo wa BAKWATA pia alitoa wito kwa vyombo vinavyosimamia uchaguzi kutenda haki na kufuata taratibu zote za uchaguzi.

"Vyama vya siasa pia epukeni rushwa kwani itasababisha kutokuwapo kwa haki," Alhaji Mruma alitoa angalizo.

Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Dk. Abubakar Zuber bin Ally, aliwataka Watanzania na waamini wa dini hiyo kulinda amani ya nchi na kuwa na maadili mema.

Mufti Zubeir aliwataka pia Waislamu na Watanzania kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa nchi, ukiwamo ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika sekta za elimu na afya, akisema, "Waislam tujenge na tulinde uchumi wetu, tusomeshe watoto ndani na nje ya nchi."

Vilevile, Mufti alitoa wito kwa Watanzania kuwa wazalendo na kulinda nchi yao, akisisitiza kuwa "kufanya hivyo ni wajibu wa kila mmoja, tuichunge na tuipende nchi yetu, ni muhimu kwa kila Mtanzania kushiriki katika kuzuia mmomonyoko wa maadili."

Akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Baraza hilo, Waziri Mkuu Majaliwa alisema kuwa wakati huu ni muhimu kwa nchi kushikamana na kuwa wamoja katika kulinda amani ya nchi kuelekea uchaguzi.

Kuhusu matukio ya utekaji na mauaji yanayoendelea nchini, Majaliwa alisema serikali inaendelea kukabiliana nayo na kuwa tayari Rais Samia alikwishaunda Tume ya Haki Jinai inayoshughulikia masuala yanayoendana na hayo, hivyo kuwataka Watanzania kuendelea kuwa na imani na serikali yao.

"Kuna baadhi wameanza kuleta chokochoko katika taifa hili, lakini hatua kali zitachukuliwa. Suala muhimu ni kila mmoja awe mlinzi wa mwenzake na pale linapotokea suala linalotiliwa shaka, litolewe taarifa mapema iwezekanavyo," aliagiza Majaliwa.

Waziri Mkuu alitoa wito kwa viongozi wa dini na Watanzania kwa ujumla wahakikishe wanasimamia na kuimarisha maadili mema kwa jamii ili kuepuka maovu na kuleta maendeleo endelevu nchini.

"Nitumie fursa hii kuendelea kutoa rai kwa wananchi, wazazi na viongozi wa dini kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika malezi ya watoto wetu katika ngazi zote kwa kuzingatia maadili na tamaduni ya taifa letu. Ni wajibu wetu kama wananchi," alisema.

Majaliwa alisema kuwa viongozi wa dini wana jukumu la kutoa mwongozo na malezi ya kiroho kwa waumini kwa kuwa wana nguvu kubwa ya kuhamasisha maadili na tabia nzuri.

"Wazazi, ninyi mna jukumu la msingi katika kulea watoto wenu kuanzia katika ngazi ya familia ili kujenga tabia njema, na tukifanya hivyo matendo ya ovyo hayatakuwapo, lazima tuwe macho katika matendo haya ambayo yanaweza kuleta hofu kwa jamii yetu," alisema.

Majaliwa alisema kuwa kila mmoja anapaswa ashiriki katika kulinda taifa kwa kutambua matendo yote yanayoashiria uvunjifu wa amani ili nchi iendelee kuwa imara.

"Suala la ulinzi na usalama ni letu sote Watanzania, ndivyo tulivyofanya tangu Tanzania ipate uhuru," Waziri Mkuu alisema.

Aliwataka waumini wa dini ya Kiislamu kutumia sherehe za Maulid kwa kuonesha kwa vitendo namna ya kuishi kwa upendo, heshima, maadili, huruma na uadilifu.

"Kwa kuenzi maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W), tutumie sherehe za Maulid kuwa chanzo cha mabadiliko chanya katika maisha ya waumini. Sote tutumie nafasi hii kuhamasika na kujitahidi kuishi kwa maadili ya Mtume, ambayo yanajumuisha tabia nzuri, uadilifu na huruma," alisema.

Rai ya BAKWATA kuhusu kuundwa tume huru ya kuchunguza matukio ya utekaji na mauaji nchini, imetolewa siku moja baada ya

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kuunga mkono hoja ya kuchunguza matukio hayo.

Ikiwakutanisha viongozi wandamizi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mkoani Dar es Salaam juzi, TEC ilionya kuwa tunu za undugu na amani nchini zimeshambuliwa kutokana na matukio ya kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa Watanzania yanayoendelea.

Viongozi hao ni Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi.

Akiwatambulisha viongozi hao juzi kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, alisema walikwenda kushiriki Kilele cha Kongamano la Tano la Ekaristi Takatifu la Kitaifa.

Padri Kitima aliwaita na kuwasimamisha kwa pamoja viongozi hao jukwaani kuwatambulisha kisha aliwakumbusha kuwa wao ni ndugu, hivyo wakaishi kwa upendo, wakapeleke tunu ya injili na kusambaza upendo katika vyama vya siasa.

Alisema historia ya viongozi inaonesha kuwa walilelewa kwenye misingi ya kikatoliki, hivyo wakaienzi Ekaristi kwa kuendeleza upendo na undugu.

Makamu wa Rais wa TEC, Askofu Eusebius Nzigilwa, alisema kuwa hivi sasa tunu za undugu na amani ya nchi zimeshambuliwa kutokana na matukio ya kuteka, kutekwa, kuumizwa na kuuawa Watanzania.

Alisema Tanzania kwa miaka mingi inajulikana kama kisiwa cha amani, udugu na mahali pekee Afrika ambapo raia wake wameendelea kuishi kwa umoja, amani na undugu licha ya tofauti zao za kikabila, kiimani, kiitikadi na kiuchumi.

"Tunajiuliza nini kimepotea kwenye tunu yetu hii? Taifa letu limepotea wapi? Je, uongozi na mamlaka husika pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimezidiwa nguvu na maarifa hata kushindwa kudhibiti hali hii?" alihoji.

Alisema TEC haiamini kama makundi hayo ya kihalifu yana nguvu kuliko vyombo vya ulinzi na usalama na kuviomba vitimize majukumu yao, ili kurudisha heshima ya taifa ya kuwa kisima cha undugu na amani.

"Tunaunga mkono wito wa viongozi na watu mbalimbali wa kufanyika uchunguzi wa kina na haraka, ili wale wote waliohusika na matukio hayo yafikishwe mbele ya sheria," alisema.

HABARI KITAIFA

## Fedha zatengwa kujenga madaraja yaliyoharibiwa na El-Nino, kimbunga

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imesema inatarajia kujenga daraja la mita 100 eneo la Mto Mbwemkuru mpakani mwa wilaya za Ruangwa na Kilwa pamoja na Daraja la Nakiu (mita 70) mkoani Lindi katika mwaka huu wa fedha.

Lengo la ujenzi huo ni kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa mkoa huo.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Godfrey Kasekenya, alieleza hayo juzi wakati akikagua miundombinu ya barabara na madaraja mkoani humo.

Akiwa eneo hilo, Kasekenya alisema daraja la zamani ambalo limeharibiwa na mvua ya El-Nino na kimbunga Hidaya iliyonyesha mwanzoni mwa mwaka huu, litakarabatiwa na kutumika kwa muda wakati ujenzi wa daraja jipya ukiendelea.

Kasekenya alisema: "Tutajenga daraja lenye urefu wa mita 100 hapa kutokana na ukubwa wa mto huu, tupo katika hatua za ununuzi za kumpata mkandarasi wa kujenga daraja hili, hivyo wananchi wa Lindi msiwe na wasiwasi kwani fedha zilishapatikana za kurudisha miundombinu hii."

Aliongeza kuwa ujenzi wa daraja hilo unakwenda sambamba na ujenzi wa barabara ya Mtwara - Dar es Salaam pamoja na madaraja mengine yaliyoharibiwa na mvua hiyo na kimbunga Hidaya na kusisitiza kuwa hatua za kutafuta makandarasi zinaendelea na ujenzi wake unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack, alipongeza Wizara ya Ujenzi kwa juhudi walizofanya, ikiwamo kurejesha mawasiliano kwa madaraja na barabara zilizoathiriwa na mvua ya El- Nino na kimbunga Hidaya mkoani humo kwa muda mfupi.

Zainab alisema: "Nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali yake kutenga fedha kwa ajili ya kurejesha miundombinu hii, Wizara ya Ujenzi imekuja kufanya tathmini kuona maeneo yaliyoathirika, ninaamini utekelezaji utaanza mapema."

Mvua ya El-Nino iliyonyesha mwaka jana, ilisababisha athari kubwa ya miundombinu katika mikoa mbalimbali nchini hususani mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani.



Diwani wa Kata ya Gwata, Zongo Reuben, akizungumza jana katika mazishi ya kijana, Costa Clemence (22) mkazi wa Kijiji cha Maseyu, wilayani Morogoro anayedaiwa kuuawa na watu wasiojulikana. **PICHA: IDDA MUSHI**

# ACT-Wazalendo yalia na serikali utekelezaji maazimio ya Kikosi Kazi

**Na Halfani chusi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuboresha msingi wa demokrasia kwa kuzingatia maazimio ya Kikosi Kazi ambayo yaliweka mikakati ya kuponya nchi.

Pia kimependekeza kurejeshwa upya mjadala wa katiba mpya ili kupata katiba itakayojali zaidi misingi ya demokrasia, kikisisitiza iliyopo inampa mamlaka makubwa Rais.

Hayo yalisemwa jana na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita, alipozungumza na wananchi wa Kawe, wilayani Kinondoni katika mwendelezo wa mikutano ya hadhara ya chama hicho maeneo mbalimbali nchini.

Alisema demokrasia ya nchi hivi sasa ipo mikononi mwa Rais, inategemea siku atakavyoamka, jambo ambalo alisisitiza ni misingi ya utawala wa kikoloni.

"Kama tunazingatia demokrasi yetu, ni muhimu tukaijengea misingi ya kisheria kuliko ya hisani ya Rais," alisema Mchinjita.

Katika mkutano huo, Makamu Mwenyekiti pia alisema Kawe inakabiliwa na migogoro ya ardhi, akitaka serikali kuangalia namna ya kuitatua. Katika hilo, alitaja mgogoro unaohusisha kiwanda cha saruji na wakazi wa maeneo ya Chasimba, Chui na Tembo.

"Tunataka serikali ihakikishe maeneo hayo yanabaki kwa wananchi na ipeleke mpango wa kurasimisha maeneo yao ili waishi kwa amani," alisema.

Mchinjita pia alikemea kitendo cha baadhi ya aliowaita "vigogo wa serikali" kugeuza makazi Hifadhi ya Bahari Mbweni kwa kukata mikoko na kufanya makazi yao na kwamba kitendo hicho kinakinzana na mpango wa serikali wa kutunza mazingira.

"Wamekata mikoko ekari tano, na viongozi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wakipigiwa simu na BMU ambao wamekabidhiwa jukumu la ulinzi wa fukwe wanagoma kutoa maelezo ya nini kimetokea," alisema Mchinjita.

Katika mkutano huo, Makamu Mwenyekiti alidai Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimekosa mbinu mbadala ya kukabiliana na mafuriko katika Jimbo la Kawe ambayo maeneo yake yanaathiriwa, yakijumuisha Tegeta, Mbweni, Ununio, Boko, Bunju.

Mchinjita alisema hali hiyo imetokana na ubovu wa mipango miji iliyowekwa na serikali, akitaka serikali ikate Msitu wa Mabwepande na igawe maeneo kwa wananchi ambao hukumbwa na mafuriko na wawezeshwe ujenzi ili kuwakomoa na adha hiyo.

"Lengo letu kama chama cha upinzani, tunataka serikali iliyoko madarakani itafute suluhu ya makazi kwa wananchi wake. Pia iwajibike kwa kuwasaidia wananchi hao ambao msaada pekee wanaopewa na wakati wa mafuriko ni kuambiwa wamejenga bondeni. "Viongozi wanapaswa kutafuta suluhu ya matatizo yanayowakabili raia, lakini yapo mambo ambayo ni kielezo cha wazi kwamba serikali ya CCM imeshindwa kuongoza taifa letu.

"Leo ukienda hospitali za serikali, jambo la kwanza utakalokutana nalo ni uhaba wa wahudumu wa afya, madaktari, vifaa tiba, dawa. Pamoja na upungufu huo, bado gharama za matibabu ni kubwa," alisema. Akihitimisha mkutano wake, aliwaomba wananchi wa Kawe kukiunga mkono chama hicho ili kije na mbinu mbadala za kutatua matatizo yao ambayo hayajatatuliwa na serikali ya CCM.


ARM AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGEMENT CO LTD

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **MuCoBa Bank Plc** TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA **TAREHE 17-09-2024** NA KUENDELEA KUTAKUWA NA MARUDIO YA MNADA WA HADHARA WA KUUZA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA.

| NO | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA/ MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | KELVIN LEONARD MBEMBATI | HOTEL NA LODGE | MJI MDOGO WA ILULA "KITONGOJI CHA MASUKANZI" MKOA WA IRINGA, WILAYA YA KILOLO BLOCK "B" PLOT No 1 L.O. No 1396478 | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 2. | AMOS SANGA | NYUMBA | IRINGA - ILULA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 3. | METHEW NALOLE | PAGALE | MAFINGA - CHANGARAWE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 4. | JOEL PETER MAKOLO | NYUMBA | MADIBILA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 5. | LUSANI LUTEGO | NYUMBA NA SHAMBA | NYOLOLO - IHANGANATWA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 6. | CHARLES MASHITA | NYUMBA | MAFNGA - IHONGOLE | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 7. | MARRY NGELULA | NYUMBA | MAFINGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 8. | FABIAN GODFREY YERINDE | NYUMBA | KATA YA BOMA-IHONGOLE (MAFINGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 9. | ISAYA CUPPUSWAMY | NYUMBA | MAFINGA – WAMBI LUGANGA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 10. | MENERICK BEATUS BALAMA | NYUMBA | IRINGA – KILOLO | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 11. | GAUDENCE CHARLES MOHELE | NYUMBA | MADIBILA | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 12. | VAILETH GEORGE HAULE | NYUMBA | MAKWAWA -LUNGEMBA (MAFINGA) | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |
| 13. | MENERICK BEAUS BALAMA | NYUMBA | KILOLO- IRINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 14. | LUKAS LEVIS MSINGWA | NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE-MTAA WA BLOCK J (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 15. | IBRAHIM KIYEYEU | NYUMBA | UPENDO - MGODI | KUANZIA SAA 3 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA (25%) AU ZAIDI BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI (75%) ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA.

**MAWASILIANO: +255 719 779998/ +255 780 303984**
**WANANCHI WOTE MNAKARIBISHWA SANA**




Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wa pili kushoto), akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Pwani, Mhandisi Baraka Mwambage (wa pili kulia), alipokagua ujenzi wa barabara ya Nyamwage – Utete (Km 33.7) kwa kiwango cha lami mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. **PICHA: UJENZI**

# Wakulima wa tumbaku walalama kulazimishwa kutia saini mikataba

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku katika Mkoa wa Tumbaku Kahama wamedai kulazimishwa kuingia mikataba ya miaka mitatu na kampuni za ununuzi wa tumbaku na baadhi yao wamegoma kuridhia mikataba hiyo wakidai ni ya kinyonyaji.

Imeelezwa kuwa wakulima hao wanahofia kuendelea kunyanyaswa na kukandamizwa, ikiwamo kucheleweshewa malipo.

Udadisi wa mwandishi wa habari hii umebaini kuwa wanaogoma kufunga mikataba hiyo, wanatishiwa kufutwa na vyama vyao vya msingi pamoja na kuondolewa madarakani kwa viongozi wao.

Mwandishi pia amebaini mikataba iliyofungwa kati ya wakulima na kampuni wanazozitaka wakulima, haitambuliwa hali kadhalika kunyimwa na pembejeo za kilimo zinazotolewa kwa ruzuku ya serikali.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Shilabela Balemi AMCOS 2018, Amos Masanja, alisema jana mjini hapa kuwa wakulima wamegoma kufunga mikataba ya miaka mitatu ya kulazimishwa kuwa chini ya kampuni za ununuzi wa tumbaku.

Alidai kampuni hizo zinapigiwa debe na viongozi na kuwaletea waraka na barua za mashinikizo ya kuridhia mikataba hiyo bila kutoa uhuru kwa wakulima wachague kampuni wanayotaka kufanya nayo biashara.

"Chama cha Ushirika ni muungano wa watu waliojiunga pamoja kwa hiari kwa madhumuni ya kufanikisha mahitaji yao kwa kuanzisha na kumiliki chombo chao kidemokrasia na kuchangia mtaji unaohitajika kwa usawa na kukubali kuyakabili matatizo na kupata manufaa kutokana na shughuli zake ambazo wao hushiriki kikamilifu," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imefanya mambo mengi mazuri kuhakikisha inawainua wakulima na kuwawezesha kulima kilimo chenye tija kwa kuwapatia masoko kwa kuwaletea kampuni nyingi za ununuzi wa tumbaku ili kuleta ushindani miongoni mwa kampuni.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo, serikali imetoa fursa kwa wakulima kufanya uchaguzi wa kampuni za kufanya nazo biashara.

Hata hivyo, Masanja alisema jitihada hizo zinakwazwa na wanachokilalamikia - wanalazimishwa na kuchaguliwa kampuni za kufanya nazo kazi.

"Suala la kuingia mikataba ya miaka mitatu limekuja ghafla na kuwapo kampuni nyingi kufanyike kwa kujinadi kwa AMCOS na wakulima na ziende na sheria za ushirika ambazo zinaelekeza mwanachama ndiye mwenye uamuzi wa kuchagua kampuni kwenye mikutano ya vyama.

"Na tukifunga mikataba ya miaka mitatu na kampuni moja, kampuni zingine zitapata wapi vyama na hizo kampuni nyingi za ununuzi wa tumbaku zilikuja kwa ajili gani?

"Wanataka kuturudisha nyuma, kampuni zilipokuwa chache na mkulima alikuwa anapangiwa kiasi cha kuzalisha. Suala hili halikuja kwenye mrengo wa kumnufaisha mkulima," alilalama Masanja.

Alirejea barua kutoka bodi ikielekeza kufunga mikataba ya miaka mitatu (2024/25, 2025/26 na 2026/27) na vyama vyote vya msingi kuendelea kufanya biashara na kampuni walizouzia tumbaku msimu uliopita. Alisema kuwa imeelekezwa kuwa kila chama kibaki na kampuni yake waliyonunua tumbaku msimu uliopita ili kampuni iweze kufanya uwekezaji mkubwa.

Emanuel Maziku, mkulima na kiongozi wa Chama cha Msingi Kazana AMCOS cha wilayani Kahama alisema "zamani tulikuwa tunatia saini mikataba ya miaka mitatu, lakini tulikuwa tunaihuisha kila mwaka. Ilikuwa fursa ya pande zote mbili - kampuni na vyama kubaki kuendelea kuwekeza katika hicho chama na kutoa fursa kwa chama kuihama kampuni. Mikataba ya sasa haitoi mwanya huo.

"Mikataba imekuwa shida, vyama vimekosa uhuru wa kufanya uamuzi wao kwa mujibu wa taratibu na sheria za ushirika. Umelima na kampuni imekunyanyasa, imekucheleweshea malipo mpaka unaingia msimu mwingine hujalipwa na umekubaliana malipo kufanyika kwa dola, kampuni inakubadilikia na kukulipa kwa shilingi, unalazimishwa kuendelea nayo."

Dotto Shinji kutoka Chama cha Msingi Isungasabo, kijijini Kangeme, Kata ya Ulowa, alisema kumekuwa na ucheleweshwaji malipo ya wakulima unaofanywa na kampuni za ununuzi wa tumbaku kinyume cha sheria za ushirika.

Alisema sheria inataka wakulima walipwe ndani ya siku 14 tangu kuuza tumbaku, lakini malipo yamekuwa yanacheleweshwa hata kwa zaidi ya miezi.

Ofisa Kilimo Halmashauri ya Ushetu, Elibariki Ndau, alisema wanasimamia maelekezo ya wizara, hivyo ni lazima mkulima ahamasishwe kufunga mikataba hiyo.

## Wakala adaiwa kutoweka zaidi ya wiki, mama adai alikuwa akifuatilia madeni

**Na Samson Chacha,** TARIME

MFANYABIASHARA wa uwakala wa fedha za mitandao ya simu, utunzaji na ukopeshaji mjini Tarime, Kevin Masige anadaiwa kutoweka kwa zaidi ya wiki moja, hali iliyozua taharuki ikihusishwa na vitendo vya utekaji.

Akisimulia kutoweka kwa kijana wake, Mama yake Mzazi, Emakulata Masige, Muuguzi wa Hospitali ya Wilaya Tarime, alisema wameshatoa taarifa polisi na kwamba kijana wake aliwapigia simu mwishoni mwa wiki kisha akakata.

Alidai kuwa Jumatatu Septemba 9, mwaka huu, saa kumi jioni, kijana alifunga duka na kuondoka kwenda Buhemba, nje kidogo ya Mji wa Tarime akidai anakwenda kufuatilia madeni ya fedha za mikopo kwa wateja wake.

"Kijana wangu hakurejea nyumbani tangu siku hiyo. Tulimaliza siku mbili pasipo kumwona, tukaenda kutoa ripoti Kituo cha Polisi Tarime, tulijaribu mara kadhaa kumpigia simu bila mafanikio kisha kuwataarifu ndugu na marafiki zake, wakiwamo wateja wake ili kutoa taarifa watakapomwona," alisema Masige. Alidai kuwa Ijumaa iliyopita, kijana wake alipigia simu dada yake anayeishi jijini Mwanza, Magreth Masige, akidai yuko salama na baada ya muda mfupi alikata simu hiyo. "Tulijaribu kumwuliza binti yetu huyo aliyempa simu kutupigia kuwa 'yuko wapi huyo Kelvin?', alisema kuwa aliondoka baada ya kupiga simu na hakujulikana tena aliko," alisema mama huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya, SACP Michael Njera, alithibitisha kupokea kwa taarifa hizo na kuwa zilitolewa katika Kituo cha Polisi Tarime na wanaendelea kufuatilia suala hilo.

Alimtaka mfanyabiashara ajitokeze na kuongea na wazazi wake ili kuondoa taharuki kwa familia na jamii.

# Manufaa kongamano ufuatiliaji tathmini yabainishwa

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Dk. Jim Yonazi, amesema kongamano la ufuatiliaji na tathmini litatoa fursa kwa wadau wote, ikiwamo serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi kushirikiana katika kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji ambayo itachochea maendeleo nchini.

Aidha, alitoa wito kwa wadau katika sekta hiyo na Watanzania kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika kongamano hilo la tatu la wiki ya ufuatiliaji, tathimini na kujifunza linalotarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Septemba 20, mwaka huu, visiwani Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na kiongozi huyo, kongamano hilo la kitaifa nchini limekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha eneo hilo serikalini kwa kuongeza uwezo wa wataalamu wa ufuatiliaji na tathimini.

"Kupitia warsha hiyo, mafunzo, na midahalo, washiriki hujifunza mbinu mpya, zana na teknolojia za kisasa za ufuatiliaji na tathmini ambazo zinaweza kutumika kuboresha utendaji wa miradi ya maendeleo," alisema Dk. Yonazi.

Kongamano hilo pia linalenga kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa sera na miradi ya maendeleo, kwa kuleta pamoja wadau mbalimbali wakiwamo watendaji wa serikali, wabunge, mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi.

Alisema kongamano hilo linatoa fursa ya kujadili jinsi ufuatiliaji na tathmini inaweza kutumika kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na uwajibikaji.

Umuhimu wa ufuatiliaji na tathmini katika maendeleo ya nchi na inachangia kwa namna mbalimbali kuboresha utendaji wa serikali na sekta binafsi.

"Ufuatiliaji na tathmini husaidia kubaini jinsi rasilimali zinavyotumika na kuhakikisha kwamba fedha na muda zinalenga malengo yaliyokusudiwa hii inasaidia kuongeza uwazi katika utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo.

"Kwa kutumia data sahihi, watunga sera wanaweza kuchambua jinsi programu za maendeleo zinavyotekelezwa na matokeo yanayopatikana, hii husaidia kufanya maamuzi ya sera yaliyo sahihi zaidi kwa kuzingatia ushahidi wa kiutendaji," alisema Dk. Yonazi.

Hata hivyo, alisema matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanawezesha serikali na wadau wa maendeleo kupima mafanikio na changamoto za miradi mbalimbali ya maendeleo, pia yanatumika kurekebisha au kuboresha programu zinazoendelea kutekelezwa.

Vile vile, alitoa wito kwa wadau mbalimbali kushiriki ili kuongeza uelewa wa masuala ya ufuatiliaji na tathmini, kupata maarifa ya ubunifu pamoja na kushirikishana uzoefu katika eneo hilo nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi Serikali za Mitaa uwaibue wanawake

**UCHAGUZI** wa serikali za mitaa unatarajia kufanyika mwezi Novemba mwaka huu na uchaguzi huu uwe chachu ya kuwaibua wanawake wengi kushiriki kuwania nafasi za uongozi.

Wakati wa wanawake kutumika kama wapiga kampeni na kuwa ngazi za kupandishia wenzao kugombea nafasi hizo umepitwa.

Ni haki ya kila mmoja kushiriki kupiga kura na kuchaguliwa hivyo wanatakiwa kuamka na kujitokeza kwa wingi.

Huu ni wakati wa kuonesha kuwa wanawake wanaweza kupambana na kushinda kwenye chaguzi kutokana na watakavyoweza kujieleza na kumwaga sera zao.

Kukatishwa tamaa kuwe mwiko kwao na wasikubali kuwekewa vikwazo vya aina yoyote ile.

Wengine wanakosa ujasiri wa kuthubutu baada ya kuona wenzao wanavyopata misukosuko ikiwamo kudhalilishwa na kutukanwa kwenye majukwaa. Hali hiyo inathibitishwa na baadhi ya viongozi wanawake waliowahi kushika nyadhifa za juu serikalini na kwenye taasisi mbalimbali, mikikimikiki waliyopambana nayo mpaka kufanikiwa kushika uongozi.

Miongoni mwa sababu zinazowadhoofisha wanawake wengi kujitokeza kuwania nafasi iwe kwenye siasa au taasisi ni kuombwa rushwa ya ngono.

Kuna wanawake wanaojitambua ambao wakishatajiwa suala la rushwa ya ngono, anaona isiwe tabu na kuamua kuendelea na mambo mengine. Sehemu yoyote linapokuja suala la kupewa nafasi kwa upendeleo, ufanisi hukosekana kwa sababu ya kukosekana heshima.

Hii ni vita kubwa na inapaswa kukomeshwa na wanawake wenyewe kwa kujitambua na kutokubali kudhalilishwa kwa namna yoyote ile.

Kwenye nafasi za kisiasa, wanawake wengi hulalamika kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji kwa kuitwa majina ya ajabu ajabu ili tu wakatishwe tamaa. Kwa wanawake walio kwenye ndoa wanakuwa kwenye mtihani mkubwa baada ya wenza wao kusikia yanayofanyika kwenye mchakato wa kuwania nafasi hizo na kuamua kuwakataza ili kuepuka kashfa.

Suala hili linahitaji kukemewa na pia elimu ya kutosha kuanzia mijini na vijijini ili wanawake wengi waelimike na kujitokeza kuwania nafasi.

Vyama vya siasa, wanaharakati wa haki za binadamu mna kazi kubwa ya kutoa elimu kupiga vita jambo hilo.

Kwa kudhoofisha wanawake kujitokeza kuwania nafasi za uongozi, kunaweza kukapoteza ari yao ya kuonyesha vipaji vyao vya uongozi.

Na katika maeneo mengi ya kazi imeshuhudiwa kuwa wanawake wanapopewa uongozi wanafanya vizuri na hata suala la rushwa ya ngono huwezi kulisikia. Mapambano ya rushwa ya ngono ni lazima yawe makubwa ili kukomesha hali hiyo kabisa.

Aidha, wanawake wajitahidi kuhamasishana wajitokeze kugombea nafasi mbalimbali wasibakie kuwa wapigakura.


Katiba inaruhusu kugombea, kupiga kura na kupigiwa, lakini bado hawajitokeza kwa hofu ya udhalilishaji.

"Vikwazo vipo vingi vinavyowafanya wanawake washindwe kujitokeza kugombea, sababu moja wapo hatuna uthubutu, pili, elimu ya uraia haiwafikii kinamama nje ya miji, juhudi zifanyike wafikiwe. Rushwa ya ngono ni kikwazo, waume zetu wakisikia unataka kugombea wanakukataza kama haujaolewa wazazi wanakukataza kugombea," anasema aliyewahi kuwa waziri wa zamani Shamim Khan.

Mwanamke akitaka kugombea nafasi yoyote anapaswa kukataa rushwa ya ngono na akiwa na heshima yake hakuna atakayemfuata.

Pia, ni muhimu wakajua kanuni na vyama vya siasa vifanye bidii kupeleka kanuni hizo hadi ngazi ya chini ndipo watapatikana wanawake wengi. Kuna nafasi za viti maalum vya udiwani na ubunge, ambazo zimependekezwa na wadau wa siasa ziwe na ukomo wa miaka kumi ili kutoa nafasi kwa wanawake wengine kuziwania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Tukiacha mazoea hatutalia njaa

**MWAKA** jana Rais Samia Suluhu Hassan, akiwahutubia viongozi wa Afrika kwenye jukwaa la kilimo (AGRRF 2023), anawaambia lazima marais wahakikishe Afrika inajitosheleza kwa chakula.

Ni katika kusanyiko linaloangazia umuhimu wa kuwekeza katika kilimo biashara ili kulinusuru bara hili na njaa na wakati mwingine uhaba wa chakula usiokuwa na sababu.

Anasema Afrika inajulikana kuwa ina asilimia 65 ya ardhi inayofaa kwa kilimo, yapo mabonde na nyanda za kilimo na ufugaji, vipo vijito na mito mikubwa inayofanikisha umwagiliaji.

Sifa hizo zinathibitisha kuwa Afrika haikustahili kulia njaa wala kuagiza ngano, mahindi au nafaka ya aina yoyote kutoka nje.

Rais Samia anahutubia jukwaa la chakula Septemba mwaka jana ambapo leo umetimia mwaka mmoja wa AGRF 2023, ambao unaamsha hamasa za kuwa na suluhu ya changamoto ya chakula hasa kwa kujitosheleza kwa kila namna.

Tukiangalia Tanzania asilimia 60 ya raia ni vijana ambao ni nguvu kazi ambayo inahitaji kula vizuri na kupata lishe bora ili kufanyakazi ya kuibadili nchi kutoka kwenye umaskini kwenda kwenye utajiri unaoambatana na kujitosheleza kwa chakula.

Ni wazi kuwa juhudi zinafanyika kuwa na chakula cha kutosha na kama serikali inavyoeleza bungeni, Tanzania inajitosheleza kwa chakula ikiwa na zaidi ya asilimia 130 ya nafaka muhimu hasa mahindi na mchele.

Baadhi ya nafaka hasa mahindi huuzwa ukanda wa kusini mwa Afrika kuanzia Zambia na Malawi zinazokabiliwa na njaa.

Ni jambo jema kwa sababu nchi ina mahindi na mchele, hata hivyo wakati umefika kubadilika na kuachana na ulaji wa kimazoea.

Ni vyema kusahau fikra kuwa chakula ni lazima kupata unga wa mahindi kwa ajili ya ugali au mchele ili kupika wali na ngano kutengeneza vitafunwa kuanzia mkate, chapati hadi maandazi.

Tukumbuke kuwa tatizo la kutegemea nafaka moja kama mahindi kwa ajili ya sembe na dona kunasababisha wakati mgumu kwa wananchi sembe inapopanda bei, hasa pale mahindi yanapopungua nchini.

Hamasa ianze sasa Watanzania waanze kuzoea kuchanganya nafaka na mazao mengine mfano mtama, mhogo, viazi na magimbi kupata unga.

Siyo lazima kula ugali wa sembe muda wote, wakati mihogo inaozea shambani. Uwepo unga wa mchanganyiko huo na zifanyike hamasa kubadili mazoea ya unga wa aina moja pekee.

Pia, si lazima kula chapati au vitafunio vya ngano pekee tubadili fikira tuanze kuzichanganye na unga wa ndizi, viazi, vitamu, mbatata, dengu na muhogo.

Kadhalika maandazi nayo mambo yabadilike kuwe na vitafunwa vya unga wa nafaka mbalimbali kupunguza utegemezi wa unga wa aina moja.

Kutegemea ngano pekee kunasababisha Tanzania na Afrika kulia kila siku kuwa kuna uhaba wa nafaka hiyo inayoagizwa kutoka Ukraine na Urusi.

Licha ya rasilimali au nafaka nyingi zilizopo Watanzania wamebaki kulalamikia kukosa chakula au kushindwa kumudu milo mitatu wakati kila kitu kipo.

Si lazima kula wali unaotokana na mchele hata wa mtama unawezekana, mahindi na ngano pia. Kutegemea maharage muda wote kunasababisha yafikie kilo moja Shilingi 4,000 hasa mijini, inakuwaje watu wasile mbaazi, kunde, choroko, njugu mawe au dengu?

Kuwa na chakula cha kutosha siyo suala la kutegemea mataifa yaliyoendelea wasomi na wataalamu wa Tanzania wapo wabadilishe silica, mazoea ya ulaji ili kila mmoja ale na apate afya.

Ni vyema pia kila mkoa uwe na tathmini ya kujua watu au kaya zisizo na uwezo wa kumudu chakula na kutafuta ufumbuzi.

Katika mkutano wa AGRRF 2023, Rais Samia anaeleza kuwa zaidi ya watu milioni 283 wanalala njaa barani Afrika.

Katika idadi hiyo Watanzania wako wangapi? Juhudi zifanyike kuwatambua mijini na vijijini na kupata mbinu za kuwasaidia.

Aidha, kazi hiyo iende pamoja na kuhimiza mabadiliko ya mifumo ya kutumia vyakula vya aina mbalimbali ili kila mtu ale na kuondokana na changamoto ya kukosa chakula inayozungumzwa na wengi.

# Ulega agawa madume ya ng'ombe kwa wafugaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amekabidhi madume bora ya ng'ombe wa nyama 20 kwa vikundi vya wafugaji wa kijiji cha Msomera ili wasaidie kuzalisha kizazi chenye uwezo wa kutoa nyama nyingi zaidi ya wale wa asili walioko nchini.

Waziri Ulega alikabidhi madume bora ya ng'ombe wa nyama kwa vikundi vya wafugaji katika hafla fupi iliyofanyika katika kijiji cha Msomera, wilayani Handeni, mkoani Tanga, mwishoni mwa wiki.

"Tukio hili ni kutimiza mpango wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wa kuleta mabadiliko kwenye sekta ya mifugo kupitia kuboresha mbari za mifugo kwa njia ya uhimilishaji na kuwapatia wafugaji madume bora," alisema.

Alisema Tanzania inakadiriwa kuwa na jumla ya ng'ombe milioni 36.6 na kati ya hao, asilimia 97 ni wa asili. Sehemu kubwa ya uzalishaji wa nyama na maziwa hapa nchini inategemea zaidi ng'ombe wa asili.

"Ng'ombe wetu wa asili wana uwezo wa kustahimili magonjwa na hali ya mazingira ya maeneo mengi ya Tanzania. Hata hivyo pamoja na sifa hizo, ng'ombe hawa wana uzalishaji mdogo wa nyama na maziwa. Ili kuongeza uzalishaji wa nyama na maziwa, mbinu mojawapo ni kuzalisha mifugo chotara na kuboresha mazingira ya utunzaji ikiwamo lishe. Ng'ombe wa asili wana uwezo wa kuzalisha nyama kilo 80 hadi 120, lakini wakiboreshwa wanakuwa na uwezo wa kuzalisha kilo 150 hadi 200," alifafanua.

Aidha, alisema kutokana na juhudi za Dk. Rais Samia Suluhu Hassan za kutafuta masoko ya nje, soko la bidhaa ikiwamo nyama kutoka Tanzania limeongezeka kwa haraka. Mfano mauzo ya nyama nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 10,415 mwaka 2021/2022 zenye thamani ya USD milioni 42.5 hadi tani 14,701.10 zenye thamani ya USD milioni 61.4 katika mwaka wa fedha 2022/2023.

"Ili soko liwe endelevu na linalozingatia ubora wa nyama wizara inachukua hatua za kuboresha mifugo, lishe, upatikanaji wa maji na afya ya mifugo ili kuongeza uzalishaji na ubora wa nyama ikiwamo kuhakikisha kuwa wafugaji wanapata mbegu bora."

Alibainisha kuwa katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 wizara imenunua madume 200 aina ya Boran yenye thamani ya Sh. milioni 511.2 na Kijiji cha Wafugaji cha Msomera kimepatiwa madume 20.

Vilevile, alisema kuwa katika mwaka 2024/2025 wizara imepanga kununua madume 66 ya nyama aina ya Brahman kutoka nje ya nchi yenye thamani ya Sh. milioni 990 ambayo yatakopeshwa kwa wafugaji kwa mkopo wa miaka miwili bila riba kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Utaratibu wa kuwakopesha wafugaji unafanyika ili zoezi hili liwe endelevu kwa fedha hizo kununulia madume mengine.

Pia, Waziri Ulega alisema wizara yake inawahamasisha wafugaji wote nchini kuachana na ufugaji wa mazoea na kufuga kibiashara. Moja ya hatua muhimu ya kuelekea kufuga kibiashara ni kuwa na mbegu bora za mifugo zenye uwezo wa kuzalisha mazao mengi. Serikali inatoa madume haya ili yawe hamasa kwa wafugaji kuendelea kununua mbegu bora baada ya kuona matokeo mazuri ya ndama wanaotokana na madume haya.

Alisema serikali inaendelea kuhakikisha kuwa Kijiji cha Msomera kinakuwa kijiji cha mfano cha wafugaji. Pia itahakikisha kuwa mahitaji yote muhimu kwa ajili ya mifugo yakiwamo majosho, minada, vituo vya kukusanyia maziwa, machinjio, malisho na maji vinakuwapo Msomera.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akikabidhi madume ya ng'ombe kwa vikundi vya wafugaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watuhumiwa mauaji ya mjasiriamali wasakwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani hapa linaendesha msako ili kumkamata au kuwakamata waliohusika na tukio la mauaji ya Costa Clemence (22), mjasiriamali na mkazi wa Maseyu, mkoani hapa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama, mauaji hayo yamebainika Septemba 15, katika Kijiji cha Gwata wilayani Morogoro.

Kamanda Mkama alisema mwili wa marehemu ulikutwa kwenye eneo ambalo halina makazi ya watu huku mwili ukiwa umetelekezwa na pembeni yake kukiwa na pikipiki isiyokuwa na namba za usajili inayosadikiwa kuwa ni mali ya marehemu.

Aidha, kamanda alisema uchunguzi wa kidaktari unafanyika kutambua kuwa mwili huo ulipatwa na shida gani kabla ya kupatwa umauti.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wakazi wanaoishi maeneo hayo na yeyote mwenye taarifa kuhusu tukio hilo kuiwasilisha kwa polisi au mamlaka yoyote anayoona inafaa ili ushahidi uwepo katika kuwakamata wahusika wa mauaji hayo.

**KABWELA** Na Fadhili






Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia), akiwa pamoja na viongozi wa kampuni zinazoshiriki uwekezaji wa Mradi wa Madini ya Kinywe Mahenge, Morogoro wakati wa utiaji saini makubaliano ya uwezeshaji wa mradi huo, huko Afrika Kusini mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yafanikisha uwekezaji bilioni 790/- uchimbaji madini ya kinywe

**JOHANNESBURG, AFRIKA KUSINI**

BENKI ya CRDB imekamilisha makubaliano ya kuwezesha uchimbaji madini ya kinywe (graphite) huko Mahenge, mkoani Morogoro unaotekelezwa na kampuni ya Faru Graphite Corporation baada ya kupatikana dola milioni 179 za Marekani katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wake.

Mradi huo una thamani ya jumla ya dola za Marekani 290 (Sh. bilioni 790.433).

Katika mradi huo mkubwa wa madini nchini, Benki ya CRDB ambayo itatoa dola milioni 66 kati ya dola milioni 179 zinazohitajika katika awamu ya kwanza, itasimamia uwezeshaji wa kifedha kwa niaba ya taasisi zote zinazohusika na itasimamia akaunti kuu ya mradi pamoja na dhamana zote za mradi.

"Benki ya CRDB tumejikita katika kusaidia utekelezaji miradi ya kimkakati inayochochea maendeleo endelevu na kuleta matokeo yanayoonekana. Ushiriki wetu katika mradi huu wa madini ya kinywe ulioko Mahenge, unaonesha imani yetu isiyoyumba kuwekeza katika fursa zilizopo nchini.

"Mradi huu utatoa madini muhimu ya kutengenezea betri, hivyo kufanikisha upatikanaji wa ajira, uimarishaji miundombinu na kutoa fursa za biashara nchini," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela.

Ushiriki kwa Benki ya CRDB katika mradi huu ni ishara nyingine ya uwezo wa benki za ndani kufanikisha miradi mikubwa inayofanyika nchini, pia uimara wa ushirikiano kati yake na taasisi nyingine za fedha Afrika na kimataifa.

Mbali na Benki ya CRDB, mradi huo unajumuisha pia Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA) itakayochangia dola milioni 59.6 na Shirika la Maendeleo la Viwanda (IDC) nalo la Afrika ya Kusini litakalotoa dola milioni 53.4.

"Tunafurahi kutia saini makubaliano ya kuwezesha mradi huu wa Mahenge Graphite na wakopeshaji hawa wakubwa. Kukamilika kwa mchakato huu ni hatua kubwa kuelekea uendelezaji wake kwa manufaa ya wadau wote," alisema John de Vries, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Blackrock inayomiliki asilimia 86 ya hisa za kampuni ya Faru Graphite Corporation.

Mradi wa Mahenge Graphite unatarajiwa kuwa wa aina yake kwa kuleta manufaa ya kiuchumi na kimazingira kwa Tanzania na dunia nzima kwa ujumla kutokana na madini yatakayochimbwa kutoa malighafi muhimu ya utengenezaji betri, jambo litakalosaidia kupunguza uzalishaji hewa ya ukaa duniani.

Zaidi ya ajira 500 zinatarajiwa kupatikana katika mradi huu pamoja na kuchochea ujenzi wa njia ya umeme yenye kilovolti 220 kutoka Kituo cha Umeme cha Ifakara hadi eneo la Mahenge ambao utapelekwa pia katika vijiji vya karibu katika wilaya za Mahenge na Ulanga, pamoja na kutoa fursa za biashara kwa wasambazaji wa ndani, watoa huduma na makandarasi mkoani Morogoro na Tanzania nzima kwa ujumla.

# Mabweni ya wanafunzi kujengwa kwa ubia

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) kwa kushirikiana na Kituo cha Ubia wa Sekta za Umma na Binafsi (PPP), wanatarajia kujenga mabweni ya wanafunzi kwa ubia utakaogharimu Sh. bilioni 20.7.

Mkakati huo ulibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Edda Lwoga, wakati anazungumza na waandishi wa habari chuoni huko, jijini Dar es Salaam.

Alisema mabweni hayo yatakayojengwa kwenye kampasi kuu ya Dar es Salaam, yatakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,728, hivyo kupunguza pengo kubwa la malazi kwa wanafunzi.

Alisema kuwa hivi sasa kampasi ya CBE Dar es Salaam ina jumla ya wanafunzi 12,000, ambapo kwa upande wa malazi kampasi ina majengo mawili tu ya bweni yenye uwezo wa kuchukua vitanda 160 pekee vya malazi kwa wanafunzi wa kike na kiume, hivyo vinakidhi uhitaji wa malazi kwa asilimia 1.3 tu.

"Mradi huo utafanywa kwa ubia kati ya CBE na mwekezaji lakini ninaomba nitumie nafasi hii kuwafahamisha wadau, wawekezaji wa ndani na nje kuhusu fursa hii muhimu ya uwekezaji ili waweze kushiriki kwenye mkutano maalum utakaokutanisha wadau mbalimbali katika kuupeleka mradi huu sokoni na kupeana uelewa zaidi na mkutano huo utafanyika tarehe 20 siku ya Ijumaa," alisema.

Mkuu wa Chuo alisema mradi huo utakapokamilika, unatarajiwa kupunguza changamoto ya malazi kutoka asilimia 1.34 iliyopo mpaka asilimia 30 ya mahitaji ya wanafunzi.

"Hali iyopo imesababisha uhitaji mkubwa wa malazi ya wanafunzi kwa asilimia 98.6, hivyo wengi wanalazimika kutafuta malazi nje ya chuo kwa gharama kubwa, jambo linalosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kumudu gharama hizo," alisema.

Alisema chuo kimejitathmini na kuona njia ya ubia, yaani PPP, inatoa suluhisho la pengo hilo la miundombinu, hivyo kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi, CBE inaweza kutumia mitaji ya nje kujenga hosteli zinazohitajika bila kuathiri sana rasilimali zake za kifedha.

Kuhusu faida za mradi huo, kiongozi huyo alisema CBE imechagua njia hiyo ya PPP baada ya kujiridhisha na faida kadhaa, ikiwamo ni pamoja na ujenzi kukamilika kwa wakati, washirika binafsi watachangia si tu mitaji bali pia utaalamu katika ujenzi, usimamizi na uendeshaji, hivyo kuhakikisha malazi ya ubora wa juu kwa wanafunzi.

Alisema ujenzi kwa njia ya ubia utahakikisha kuwa gharama za malazi zitakuwa nafuu kulinganishwa na watoa huduma binafsi wa malazi nje ya kampasi.

"Kwa upande mwingine mradi huu unalenga rasmi kutekeleza malengo ya kitaifa, ikiwamo mipango ya serikali ya kupanua sekta ya elimu, sera ya uendelezaji wa biashara wa mwaka 2023 inayotoa kipaumbele kwa kuboresha ustawi wa wanafunzi na upatikanaji wa elimu ya juu," alisema.

# Wagonjwa moyo 60 wapokewa Muhimbili - Mloganzila kila siku

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Kitengo cha Magonjwa ya Moyo, inapokea wagonjwa 60 kwa siku, huku wagonjwa wa nje (OPD) kwa ajili ya matibabu tofauti wakifikia 1,000.

Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mfuko, aliyasema hayo Dar es Salaam baada ya Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kanu Heart Foundation, Nwanko Kanu, kutembelea hospitalini huko na kuwaona wagonjwa, wakiwamo watoto wanaosumbuliwa na maradhi ya moyo.

Alibainisha kuwa hospitali hiyo ina idadi ya vitanda 656 pamoja na vitanda 12 vya kufanyia upasuaji mkubwa; vitanda 31 vya wagonjwa mahututi katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU); vitanda 12 vya kwa ajili ya kusafisha damu 'dialysis' na vitanda 60 kwa ajili ya watoto njiti.

Alisema hospitali hiyo hutoa huduma bobezi na za kibingwa kwa wageni kutoka nchi mbalimbali barani Afrika kama vile Namibia, Rwanda, Burundi, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia.

"Tuna wauguzi bingwa, madaktari bingwa bobezi wawili katika kitengo cha moyo na mwingine amemaliza mafunzo na mmoja yuko katika mafunzo na mmoja ni daktari wa kawaida, jumla tutakuwa nao wanne.

"Wodi ya watoto ya uangalizi maalum huwa na watoto 60 kwa mara moja na muda wote hujaa. Tuna vifaa mbalimbali na vipimo vya magonjwa tofauti na vya moyo kama ECG, lakini hatuna Cathalab ambao ni maabara inayokupa uwanja mkubwa zaidi wa kufanya uchunguzi," alisema Dk. Mfuko.

Pia alieleza kuwa serikali imeweka nguvu katika kuwapa mafunzo ya ubobevu madaktari na kuwa mabingwa katika tiba tofauti, ili kupanua wigo wa matibabu, ikizingatiwa hospitali inazipokea rufani kwa wingi kutoka nchi nzima.

Kanu alisema ziara yake nchini pamoja na mambo mengine, amechagua kutembelea wagonjwa hospitalini huko, kuwaona watoto wanaougua magonjwa ya moyo.

Taasisi yangu nilianzisha mwaka 2000 na tayari watoto 690 wa Afrika wamefanyiwa upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua, ingawa upasuaji huu mara nyingi unafanyika nje ya nchi, hasa Israel, India na Uingereza.

"Nimefika hapa ili kuwatia moyo wanaougua lakini zaidi wenye matatizo ya moyo, nami nilipitia huko, ninawapa moyo kwamba watapata ahueni," alisema Kanu.





# Wakulima wa alizeti wapokea ruzuku ya mil.266/-

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

TAASISI ya Maendeleo ya Afrika (USADF), inayotoa ruzuku kwa mashirika ya Afrika, imekipatia ruzuku Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko cha Mbungwe, Dola za Marekani 100,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 266.96.

Ruzuku hiyo iliyotolewa kwa Mbungwe AMCOS ni mahususi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa zao la kimkakati la alizeti linalolimwa na wanachama 206 na wasio wanachama zaidi ya 1,000.

Akizungumza jana wilayani hapa baada ya Mbungwe AMCOS na USADF kutiliana saini mkataba wa miaka miwili wa utekelezaji wa mradi huo, Mratibu wa USADF Tanzania, Gilliard Nkini, alisema ruzuku wanayoitoa ina masharti.

"Hii ruzuku itasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya alizeti nchini, lakini mradi husika utatekelezwa kati ya Agosti mwaka huu hadi Agosti mwaka 2026.

"Ninyi wakulima mtakapofanya vizuri katika mradi huu, USADF itawaongezea Dola za Marekani nyingine 250,000 awamu ya pili ili mwendelee kuzalisha zao hili.

**"Hii ruzuku itasaidia kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya alizeti nchini, lakini mradi husika utatekelezwa kati ya Agosti mwaka huu hadi Agosti mwaka 2026.**

Zaidi aliongeza, "Hizi fedha zisije zikatumika kama dhamana ya kukopesha na trekta ikiletwa haitatumika kuchukulia mkopo mpaka masharti ya mkopo siku yakiondolewa."

Awali, Mtaalamu wa Ruzuku na Utawala kutoka USADf, Jessica Ash-Piper, alisema wao wamejikita kwenye kuongeza uzalishaji katika nchi 20 za Afrika.

Alisema alifurahia kuzinduliwa mradi ili kuongeza mnyororo wa thamani wa AMCOS hiyo.

Akieleza mambo ambayo yatafanywa wakati wa mradi wa Programu Meneja wa USADF na ADC Tanzania, Elleen Mwakisese alisema lengo la mradi ni kukuza uchumi na kuongeza uzalishaji kwa kuangalia ubora wa alizeti.

Vitu vingine alisema watawasaidia kuajiri wataalamu wa kilimo, biashara, fedha na kuwanunulia vifaa zikiwamo pikipiki, vifaa vya ofisi, mizani, vipima unyevu na kuwajengea kitalu cha miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Naye Mwenyekiti wa Mbungwe AMCOS, Lomayan Molleli, alilishukuru shirika hilo kwa kuwapatia ruzuku hiyo ya mradi wa alizeti.

Mollel alisema msimu wa kilimo wa mwaka 2023/24 AMCOS iliweza kuwapatia mbegu za alizeti wakulima kwa mkopo kilogramu 800 zenye thamani ya Sh. milioni 30.450 kutoka Kampuni ya Digital Mobile Africa (DMN).



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Teule wilayani Muheza, mkoani Tanga, Dk. Mgoye Marato (kulia), akitoa elimu kwa wananchi waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi wa awali wa kupima saratani ya matiti ili kujua hali zao na kupata matibabu bure juzi, katika Hospitali Teule Muheza, Zahanati ya Kata Kwabada na Zahanati ya Kata ya Nkumba kwa ufadhili wa Shirika la JHPIEGO kutoka Marekani chini ya Wizara ya Afya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# INEC yasisitiza umakini matumizi vifaa uboreshaji daftari

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imewataka maofisa uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura mkoani Manyara, kuongeza umakini katika matumizi ya vifaa vya kuboresha daftari hilo, ili kuepusha mikoa mingine kushindwa kuendelea kwa kazi hiyo ya kitaifa.

Mjumbe wa tume hiyo, Jaji Asina Omari, alisema hayo jana wakati wa mafunzo kwa watendaji ngazi ya mkoa, kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa Halmashauri ya Kiteto, Simanjiro na Mbulu Mjini.

Aidha, alisema kutokuwa makini katika vifaa hivyo kunaweza kusababisha athari kubwa na kukwamisha mikoa mingine.

"Vifaa hivi vimenunuliwa kwa gharama kubwa na vinategemewa kutumika katika mikoa mingine ndiyo maana tunataka viangaliwe vizuri," alisema Jaji Asina.

Aidha, Jaji Asina, alitumia fursa hiyo kuwasisitiza maofisa uandikishaji kushirikiana na tume wakati wote katika kutekeleza majukumu kwa weledi mkubwa.

Vilevile, alisema maofisa wa Teknolojia ya Habari za Mawasiliano (TEHAMA), kuwa watapatiwa mafunzo maalumu ya jinsi ya kukabiliana na changamoto za kiufundi zikijitokeza wakati wa zoezi.

Mafunzo hayo yatawaongezea umahiri na wao waweze kwenda kufundisha ngazi ya kata.

Ofisa Uchaguzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Rehema Bwasi, alisema wamejipanga vizuri kusimamia zoezi hilo la kitaifa, ambapo kwa Mbulu Mjini, wanatoa matangazo ya kuzunguka mitaani na gari la matangazo na kwenye mitandao ya kijamii.

Bwasi alisema kuwa Mbulu Mjini, wana vituo 113 katika kata zote 17 na tayari wameshapokea vifaa.

Pia alieleza kuwa zoezi limeratibiwa vizuri na wako tayari kuandikisha wananchi kuanzia miaka 18 na wengine ambao wanaboresha taarifa zao.

# Watu 400 wafanyiwa uchunguzi saratani ya matiti

**Na Steven William,**
MUHEZA

WATU 400 wilayani Muheza mkoani Tanga wamefanyiwa uchunguzi wa awali wa kupima saratani ya matiti kwa ufadhili wa Shirika la JHPIEGO kutoka Marekani chini ya Wizara ya Afya.

Mratibu wa Elimu ya Afya kwa Umma wa Wilaya hiyo, Shaban Seif, akizungumzia kampeni hiyo, alisema katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza, watu 164 wamepata huduma hiyo.

Aidha, alisema katika Zahanati ya Nkumba, kampeni hiyo pia imewafikia watu 105 na Zahanati ya Kwabada watu 131, vivyo hivyo wamefanyiwa uchunguzi.

Uchunguzi huo wa awali wa saratani ya matiti, unafanyika vituo vitatu vya Zahanati ya Kata ya Kwabada, Zahanati ya Nkumba na Hospitali Teule ya Muheza.

Seif, alisema kuwa watu waligundulika na matatizo ni 73, ambapo Zahanati ya Nkumba 13, Zahanati ya Kwabada 17 na Hospitali Teule ya Muheza 43.

Alisema kuwa waliostahiki kufanyiwa kipimo cha mashine kwa uchunguzi zaidi wa matiti walikua 38, ambapo Zahanati ya Nkumba 3 Zahanati ya Kwabada 6 na Hospitali Teule ya Muheza 29.

Kadhalika, alisema kuwa waliofanyiwa uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi jumla walikuwa 190, ambapo Zahanati ya Nkumba walikuwa 60, Zahanati ya Kwabada 61 na Hospitali Teule ya Muheza walikuwa 69.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, waliogundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya shingo ya kizazi walikuwa watu tisa.

Akifafanua zaidi kuhusu kampeni hiyo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Dk. Fani Mussa, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo, kujitokeza kufanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya matiti na shingo ya kizazi, ili kujua hali zao na kupata matibabu mapema kwa wenye changamoto hiyo.

Kwa upande wake, Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Muheza, Dk. Mgoye Marato, aliishukuru JHPIEGO kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwa kuwezesha zoezi hilo la uchunguzi wa awali saratani ya matiti bure.





# Wahofia kupata ugonjwa saratani, kifua kikuu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Segese Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameingiwa na wasiwasi ya kupata ugonjwa wa kifua kikuu na saratani, kutokana na magari yanayotumika kubeba mchanga wenye kemikali ya zebaki kuoshwa na maji yanayoelekea kwenye makazi yao.

Wamesema magari hayo yametajwa kutumika kubeba mchanga unaosadikiwa kuwa na madini ya dhahabu kutoka katika migodi midogo inayozunguka kata hiyo, ikiwemo ya Ntambalale Wisolele na kuelekea kwenye viwanda cha uchakataji wa maji ambavyo vipo karibu na makazi.

Wamebainisha hayo juzi katika kikao kazi cha kukumbusha wajibu wa kufanyakazi, kulipa kodi za serikali pamoja na kutojihusisha kwenye vitendo vya utoroshaji wa madini, kilichokuwa kimeandaliwa na taasisi ya kuendeleza uchimbaji mdogo nchini kwa kuwahusisha wachimbaji na wananchi wanazunguka migodi.

Mkazi wa Segese, Bangili Nkwabi alisema wamejawa hofu ya kupata magonjwa ya saratani na kifua kikuu baada ya magari yanatumika kubeba mchanga wenye kemikali hatari ya zebaki kuoshwa sehemu za kuoshea magari na maji yake kutiririka hadi kwenye maeneo ya biashara, makazi na bustani za mboga.

"Tuna watoto wadogo ambao wanatambaa na kucheza ovyo, magari haya yanapopita na yanadondosha mchanga huo na jioni yanaposafishwa maji yake yanatiririka ovyo mpaka kwenye maeneo yetu, tuomba serikali kuingilia kati na kudhibiti suala hili kwani wanaokuja kuumia zaidi ni watoto," alisema Nkwabi.

Ofisa Afya wa Segese, Bahati Alon, aliwaahidi wananchi kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wamiliki wa maeneo ya kuoshea magari katika mji huo, kwamba wanaosha magari pasipo kuchukua tahadhari ya kujikinga na hatari hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Patrick Mahona, alisema atafanya kikao na wamiliki wa viwanda vya kuchakata madini na kuwapatia elimu ya madhara ya zebaki.

# Samia kuzindua Chuo cha TIA Kampasi ya Mwanza

**Na Vitus Audax,** MWANZA

OFISA Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Prof. William Pallangyo amesema Oktoba 12, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuzindua Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha TIA Kampasi ya Mwanza.

Alisema hayo juzi wakati Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba alipotembelea na kukagua ujenzi wa chuo hicho akiwa ziarani mkoani Mwanza.

"Majengo haya yaliyogharimu zaidi ya Sh.bilioni 7.8 yana uwezo wa kubeba wanafunzi 2430 ukilinganisha na wanafunzi 750 waliokuwa wakihudumiwa katika majengo ya awali na mradi huu umetusaidia kupata majengo ya kudumu na kutoka katika majengo ya kukodi ambayo yalikuwa hayakidhi ongezeko la wanafunzi," alisema Prof. Pallangyo.

Kuhusu miradi ya TIA nchini, Prof. Pallangyo alisema zimetolewa zaidi ya Sh.bilioni 58.1 kwa lengo la kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi zote.

Dk. Mwigulu akizungumza baada ya ukaguzi wa chuo hicho alisema hatua hiyo ni miongoni mwa shughuli zinazoendelea kutekelezwa na serikali katika kuboresha sekta ya elimu.

Alisema chuo hicho kitasaidia kuongeza mzunguko wa fedha pamoja na kuifanya Usagara kuinuka kiuchumi na kuleta maendeleo zaidi kwa wakazi wa eneo hilo, hivyo kuwataka kuitumia ipasavyo fursa hiyo.

Baada ya kukagua mradi huo, Dk.Mwigulu alifanya mkutano wa hadhara na kuzungumza na wananchi katika Uwanja wa Amani Misungwi na kupokea kero ya uhaba wa maji pamoja na malipo ya fidia kwa wananchi.

Baada ya kusikiliza kero hizo, Dk. Mwigulu alisema kuwa serikali imezipokea na zitafanyiwa kazi.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akicheza ngoma ya Bulabo, inayochezwa na kabila la Wasukuma, kikundi cha Sungusungu, alipofika Uwanja wa Amani, wakati wa ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa mkoani Mwanza na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# RC awatwisha zigo maofisa ugani ustawi wa kilimo cha pamba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amewaagiza maofisa ugani mkoani humo kuhakikisha wanatoa elimu kwa mkulima, ili kusaidia kuimarisha ustawi wa kilimo cha pamba na kuongeza mavuno.

Alibainisha hayo juzi wakati akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Shinyanga, kuonesha kusikitishwa na kushuka kwa uzalishaji wa zao hilo mkoani humo, kutokana na wakulima kulima kimazoea na kupata mavuno kidogo.

Alisema katika msimu ujao wa kilimo maofisa hao wanatakiwa kuhakikisha wakulima wanapatiwa elimu ya kilimo chenye tija ili wapate mavuno mengi na kuimarisha ustawi wa familia zao na serikali kupata mapato.

"Msimu wa kilimo uliopita 2023/2024 ambao unaelekea ukingoni, Mkoa wa Shinyanga hatujafanya vizuri kwenye pamba, serikali ilipanga kuvuna kilo milioni 30 za pamba, lakini mpaka sasa kilo zilizovunwa ni milioni 20 na haziwezi kuzidi sana, hii ni kutokana na wakulima kutofanya kilimo chenye tija," alisema Macha.

Aidha, alisema mkulima akilima kilimo chenye tija hekali moja anauwezo wa kuvuna kilo 1,500 hadi 1,750 kama ilivyotokea kwa mkulima wa pamba huko Igunga.

Alisema lakini kilimo cha mazoea hekali moja inatoa kilo 100, 200 hadi 300, mavuno ambayo hayawezi kumwinua kiuchumi.

Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo, alisema umefika wakati sasa viongozi kulinusuru zao hilo, kwa kutoa elimu kwa wakulima kufuata kanuni bora za kilimo kupitia kwenye mikutano na vikao mbalimbali, sababu kilimo cha mazoea kilichopitwa na wakati.

Baadhi ya wakulima wa pamba wakizungumza na Nipashe, walisema licha ya elimu hiyo ya kilimo chenye tija lakini changamoto nyingine ambayo husabisha kupata mavuno kidogo ni hali ya hewa.

Walisema kuna kipindi mvua zinakuwa nyingi na kusababisha pamba kuzidiwa na maji, ambapo zao hilo hua linahitaji mvua kidogo.

# Kigahe ahimiza w'biashara ulipaji kodi kwa hiari

**Na Judith Julius,** NGARA

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amewataka wafanyabiashara nchini kuhakikisha wanachangia pato la taifa kwa kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akijibu hoja za wafanyabiashara wa Ngara katika mkutano waliotaka udhibiti wa ongezeko la biashara za magendo zisizofuata utaratibu zinazoingia nchini na kuuzwa kwa bei nafuu tofauti na bidhaa za ndani.

Baada ya kupokea hoja, aliahidi kuzifanyia kazi huku akiwataka kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi bila shuruti, ili kuiongezea serikali mapato na kusaidia utekelezaji miradi ya maendeleo na kuinua uchumi wa nchi.

Awali akizungumza katika kikao hicho Mbunge wa Ngara, Ndaisaba Ruhoro alisema wananchi wanakumbwa na adha mbalimbali za kibiashara kupitia mipaka ya Kabanga na Rusumo zinazosababishwa zaidi na kukithiri kwa biashara ya magendo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara Wilaya ya Ngara, Chrispine Kamugisha alisema kero hizo zimekuwa endelevu kwa sababu ya kubadilika kwa mifumo ambayo husababisha wafanyabiashara kufilisika.

Nipashe

# TESA

Jumanne Septemba 17, 2024

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 12

Baada ya miaka mingi ya mitihani na njaa mwaka huu shule yalisha wahitimu la 7



Ukurasa 14

Matajiri wanapojipeleka anga za mbali safari za kujirusha



Ukurasa 13

MSANII ALIYEZIKWA HAI - 2

Mama: Nilimwogopa, nawaza hata mimi pia angeweza kunitoa kafara kupata mafanikio

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Marekebisho ya Sheria Rushwa ya Ngono kumbana mwathirika, naye mtuhumiwa

• Yashangiliwa, yatajwa kuwa juhudi kukomesha unyanyasaji kijinsia

RUSHWA ya ngono kwa wanaharakati na watetezi wa haki za wanawake ni tatizo kubwa na zaidi ni ukiukwaji wa haki unaochangia kuendeleza unyanyasaji wa kijinsia na kuenea magonjwa kama VVU, UKIMWI na homa ya ini.

Rushwa hiyo inahusisha maneno au bila maneno na mara nyingine ni kujenga mazingira ili kuwaingiza wanawake kwenye kutoa ngono ili wapate huduma au haki.

Mojawapo ya kampeni zinazofanyika jijini Dar es Salaam ni 'Safari salama bila rushwa ya ngono inawezekana', iliyoasisiwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI).

Kampeni hiyo inafanyika katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke, kwa kushirikiana na wadau madereva wa bodaboda, bajaji, daladala na jamii, anasema Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth Mawinza.

Anasema inalenga kumaliza rushwa ya ngono kwa wasichana na wanawake, wanaosafiri ndani ya vyombo hivyo na popote pale.

Mkurugenzi wa Janeth anasema, kampeni hiyo imesaidia pia kuondolewa kifungu cha (10) (b) cha Sheria ya Rushwa ya Ngono cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kinachombana mtoaji wa rushwa hiyo sawa na mpokeaji.



Crispin Chalamila, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. **PICHA:MTANDAO**

"Hatua hiyo imetuongezea nguvu ya kuendelea na kampeni ya vita dhidi ya rushwa ya ngono, kwani moja ya vitu ambavyo tulikuwa tunavipinga, ni kifungu hicho na sasa kimeondoka," anasema Janeth.

Anasema, kwa muda mrefu wadau walitamani kifungu hicho kirekebishwe, kwa maelezo kuwa wanafunzi na wanawake wengi hulazimishwa kutoa rushwa ya ngono bila ridhaa yao.

"Harakati za WAJIKI na wadau wengine wakiwamo Mtandao wa Kupinga Rushwa ya Ngono Tanzania za kupinga kifungu hicho, hatimaye zimezaa matunda baada kilio chao kusikika," anasema.

Ndivyo anavyosema Janeth katika mazungumzo yake na gazeti hili jijini Dar es Salaam wakati akitoa maoni yake baaada ya kifungu walichokiwa wakilalamikiwa kufanyiwa kazi bungeni hivi karibuni.

"Rushwa ya ngono ni matokeo ya tofauti, katika madaraka kati ya mhalifu na mwathirika, anayehitaji huduma kutoka kwa mwenye madaraka hana uhuru wa maamuzi," anasema.

Anafafanua kuwa kama sheria ingeendelea kutumika jinsi ilivyo, wanafunzi na wanawake wangeumia zaidi bila hatia, kwa kuwa wengi wao wanalazimika kutoa ngono bila ridhaa yao.

"Hao wanaotoa rushwa kwa kutaka wapate unafuu katika jambo fulani, waendelee kubanwa na sheria, lakini wale ambao tumekuwa tukiwapigania wanalazimishwa kutoa ridhaa yao," anasema.

Mkurugenzi huyo anasema, kumuunganisha anayeumizwa na mwenye madaraka katika rushwa ya ngono, ili atajwe kama mtoa rushwa, si sawa bali anatakiwa kutajwa kama mwathirika wa rushwa ya ngono au shahidi.

**MTANDAO WANENA**

Mtandao wa Kupambana na Rushwa ya Ngono Tanzania, umetoa tamko, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti uliofanywa na TAKUKURU kwa kushirikiana na wanamtandao kuwa wanatambua ukubwa wa tatizo hilo kwenye jamii.

Mwenyekiti wa mtandao huo, Profesa Penina Mlama anasema, tatizo hilo liko nyumbani kwa watumishi wa kazi za ndani, wakiwa waathirika wakuu, vyuoni na shuleni, wanafunzi wakiathirika zaidi.

"Kwenye maeneo mengi ya utumishi wa umma na binafsi, maeneo ya biashara, kwenye hospitali zetu, hasa kwa wagonjwa wa kike na hata kwenye taasisi za dini kuna rushwa ya ngono," anasema Profesa Penina.

Anaeleza kuwa mtandao huo unatambua mwitikio wa elimu ya kuzuia na kupinga rushwa ya ngono umekuwa mkubwa kwa wazazi, watoto shuleni, vijana vyuoni, kwenye taasisi za kidini, waajiriwa majumbani, ofisini na katika tasnia ya sanaa na utamaduni.

"Kwa kuzingatia maamuzi ya bunge yaliyofanyika Septemba 2, mwaka huu, ambapo serikali iliazimia kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bunge, ambayo yamekuwa msimamo wa Mtandao wetu pia, tumefurahia."

Anasema aidha kufuta kifungu 10 (b) na kuacha kama kilivyo kifungu 25 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Ngono, 2007 ni hatua ya kushangiliwa.

Anasema bunge lilikwenda mbali zaidi na kuongeza wigo wa ukomo wa adhabu kwa waomba rushwa ya ngono kutoka miaka mitatu hadi 10 na faina ya Sh. milioni tano hadi 10.

"Sisi wanamtandao wa kupambana na rushwa ya ngono, tunapenda kuchukua fursa hii kupongeza wanamtandao wote

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA AMRI LUGUNGULO, KISARAWE

# Baada ya miaka mingi ya mitihani na njaa mwaka huu shule yalisha wahitimu la 7

WANAFUNZI wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Kidugalo, iliyoko mkoa wa Pwani, kwa mara ya kwanza wamepata chakula shuleni wakati wa mitihani ya kitaifa ya kumaliza elimu ya msingi.

Ni takribani miaka 10 wanafunzi wa Kidugalo hawajapata mlo na hatua ya hivi karibuni ni neema kwa vile ni kujitambua na kwa wazazi na walezi ambao wameongeza thamani katika juhudi za kutafuta mafanikio kielimu.

Shule hiyo ilikuwa haitoi chakula kwa wanafunzi kwa miaka kadhaa licha ya serikali kuelekeza watoto wapate mlo shuleni.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kidugalo, Saidi Mangu, akizungumza na wanafunzi shuleni hapo kuhusu kupata chakula, anasema wazazi na walezi wa wanafunzi wa darasa la saba wamekubaliana kuwalisha.

Shule hiyo iliyoko wilayani Kisarawe ilianza kupata huduma hiyo wiki iliyopita, wakianzisha rasmi utaratibu wa kutoa michango ya kuwapatia chakula watoto wakati wa mitihani ya kitaifa wa darasa la saba.

Anasema wanaanza utaratibu huo wa kutoa mchango wa chakula kwa wanafunzi walipofanya mitihani hiyo wiki iliyopita siku za Jumatano na Alhamisi.

Mangu anasema lengo ni kuwawezesha watoto hao waliomaliza na watakaofanya mitihani mingine kupata nguvu mwilini, kujiamini na kufaulu.

Anasema michango ya wazazi na walezi hao wakishirikiana na Diwani wa Kata ya Kurui, Mussa Kunikuni, inafanyika kwa dharura baada ya mkutano na mwenyekiti wa kamati ya shule hiyo, Ramadhani Zinga.

Jumla ya wanafunzi 14, kati yao wasichana ni sita walikabidhiwa mchele, nyama ya ng'ombe, sukari, maharage, mafuta ya kula, vitunguu, kabichi na maji ya kunywa.

Aidha, walipatiwa soda, mayai, viazi mbatata, ndizi na mihogo vyote vikiwa na thamani ya Shilingi 106,000 ambayo ni michango ya wazazi na walezi.

Vyakula hivyo vinapokelewa na wanafunzi hao mbele ya Mwenyekiti wa Kijiji Mangu na Mwalimu Mkuu, Stanslous Nyandakwa, kusudi viandaliwe kwa ajili ya mlo wa asubuhi na mchana.




Diwani wa Kata ya Kurui, Musa Kunikuni (kulia), akimkabidhi mwanafunzi wa darasa la saba chakula ili kiandaliwe wakati wa mtihani. **PICHA: AMRI LUGUNGULO**

Wanafunzi hao wanawashukuru wazazi, walezi na viongozi wakiwamo diwani na mwenyekiti wa kijiji kwa kuanza utaratibu huo wa kuwachangia chakula.

Wanawaahidi kufanya juhudi na kufaulu mitihani ili kutimiza ndoto zao za kuendelea na masomo ya juu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Kidugalo, Nyandakwa anawashukuru wazazi na viongozi wa serikali kwa juhudi hizo za kuwasaidia watoto kuwa na utulivu na nguvu za kufanya mitihani yao kikamilifu.

Mapema, baada ya kukabidhi vyakula hivyo, diwani huyo anawasihi wanafunzi hao kufanya vizuri zaidi.

"Kuweni watulivu na makini katika kujibu maswali ili kutimiza ndoto zenu kwani kila mnayemuona ana nafasi iwe mwalimu, rubani na hata mimi diwani nimepita mafanikio hayo kwa njia ya elimu," anasema.

Shule ya Msingi Kidugalo, ilianzishwa wakati wa ukoloni mwaka 1956 na wamisionari wa Kilutheri na leo inapotimiza karibu miaka 70 inakabiliwa na matatizo lukuki ikiwamo ukosefu wa chakula shuleni.

Sababu mbalimbali zinazochangia ukosefu wa chakula ni utoro na mwamko mdogo wa watoto, walezi na wawazi wa kusoma na kusomesha.

Aidha, wakati mwingine hali ya umaskini inachangia pia kuwahimiza wazazi kutoa fedha au chakula kwa ajili ya wanafunzi shuleni.

Shule hiyo ambayo wakati wa ukoloni ilikuwa ikiitwa 'bush school' hakuwa na tofauti na shule nyingine ambazo kama zilivyoanzishwa zilikuwa za matope zikiezekwa na nyasi leo zinaweza kuitwa 'mbavu za mbwa'.

Kidugalo vilevile wanafunzi wake waliianza kusoma wakikaa chini ya miembe na mikorosho.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika, likajengwa jengo jingine la udongo na kuezekwa na nyasi likiwa na madarasa mawili na sasa ni shule ya kisasa ikijengwa kwa matofali.

Wanafunzi wa shule kwa miaka mingi walifanya mitihani ya darasa la saba na la nne bila kuwa na chakula.

Kama zilivyo shule nyingine za vijijini wanafunzi hao wanapata ufaulu mdogo kutokana na sababu nyingi mojawapo ni njaa, na wengi wanatembea umbali mrefu kuifikia shule.

Juhudi za kuwapa chakula zilianzishwa mwanzoni mwa mwaka 2000, na aliyekuwa mwalimu mkuu Francis Msolwa, kwa kuanzisha mradi wa kilimo kwa ajili ya chakula.

Wanafunzi walilima mahindi kwa ajili ya kupata ugali, hatua iliyokuwa na mafanikio shule ikianza kufaulisha watoto wengi zaidi yakiwa ni matokeo ya kupata chakula cha mchana shuleni.

Baadaye mradi huo ulisimamishwa kwa madai kuwa kulikuwa kundi la watu waliokuwa wakiiba mahindi kutoka shambani hivyo utaratibu wa watoto kupata chakula shule nao ukasimama na kusababisha ufaulu kuporomoka.

Hata shamba la shule hiyo limekufa na hakuna shughuli za kilimo zinazoendelea kwenye ardhi hiyo.

> Anasema wanaanza utaratibu huo wa kutoa mchango wa chakula kwa wanafunzi walipofanya mitihani hiyo wiki iliyopita siku za Jumatano na Alhamisi.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

MSANII ALIYEZIKWA HAI - 2

# Mama: Nilimwogopa, nawaza hata mimi pia angeweza kunitoa kafara kupata mafanikio

ILIKUWA Desemba 20, mwaka 1996, Maria Asenga, alipata mtoto wake wa pili akampa jina la Salimu Mbasha maarufu Rupia, jina la usanii wa muziki.

Mama yake, anazungumzia tukio la kijana huyo kusaka mafanikio, hata kukubali kuzikwa akiwa hai mwaka 2022 katika juhudi za kupata utajiri bila kazi ngumu wala jasho.

Salimu au Rupia Boy (pichani), wiki iliyopita anaelezea mkasa huo, akisema baada ya kurekodi nyimbo kadhaa ambazo ni 'odio' (zisizokuwa video) lakini pia hazikupata mafanikio alipewa mbinu mpya za kumpaisha.

Akiwa kwenye moja ya studio Dar es Salaam anapata wanamuziki wanaomshauri kuwa atafanikiwa bila usumbufu kupitia mganga wakampa namba zake.

Anaahidiwa kuwa angempika hadi apate mafanikio makubwa kwa muda mfupi, hivyo hana haja ya kusumbuka. Jambo analolikubali.

Anawasiliana na mganga ambaye angemtajirisha kwa masharti kadhaa kuu likiwa kumlipa takribani Shilingi 700,000 na baada ya hapo angemzika na kumfukua akiwa mtu mpya kiutajiri na kimafanikio kwenye muziki bila nguvu wala jasho.

Rupia hakuwa na tatizo bila kujali kuwa hakuna mafanikio bila juhudi, akatapeliwa na kuzikwa hai, jambo ambalo bila jitihada za marafiki angeweza kupoteza maisha.

Mama yake mzazi, anazungumzia kisa hicho akisema ni jambo linalomshangaza mno:

"Nilimwambia kama unakubali kuzikwa hai kaburini, hata mimi mama yako unaweza kunitoa kafara ili kusaka mafanikio."

Rupia ni mtoto wa pili wa Maria Asenga, mkazi wa Tabata Kimanga, Dar es Salaam, anayemiliki mgahawa akiuza vyakula na vinywaji baada ya kuondoka Mwanga mkoani Kilimanjaro muda mrefu.

Anasema mtoto huyo amempata pamoja na mfanyabiashara wa madini Mererani (jina tunalo), na kwamba amelelewa na kutunzwa na familia yake na ya mwenza wake, kila mmoja akitamani asome.

Anasema, Rupia alipenda muziki tangu utotoni na kwamba akiwa Sekondari ya Kileo iliyoko Mwanga, anazama zaidi kwenye muziki.

"Namwambia mwanangu shika moja soma. Uko shule lakini umekwenda mitaani unaimba na kurekodi muziki kwanini usimalize masomo kwanza?" anasema Maria.

Anaongeza kuwa anaanza kurekodi 'odio' akiwa sekondari na kila siku hamu ya kuwa mwimbaji mkubwa inaongezeka rohoni mwake.

Anasimulia kuwa Rupia au Salimu hakumweleza kuhusu safari ya kwenda kwa mganga kusaka mafanikio, ila alishtuka kumwona akiwa taabani, baada ya kunusurika na kifo kilichotokana na mauzauza ya mganga.

"Nilishangaa kupata taarifa hizo kuwa amezikwa hai na ameokolewa na marafiki, anatibiwa na nikapaswa kugharamia matibabu."


Anasema mshtuko huo umeathiri maisha yake kiasi cha kupata shinikizo la juu ya damu na kwamba kama angemweleza mpango huo angeukwamisha.

"Ilifika kipindi hata mimi namwogopa nawaza usalama wangu. Ni jambo lililonishtua mno." Anasema Maria.

Anaeleza kuwa baada ya kupata ushauri na mausia ya marafiki na ndugu, Rupia amebadilika na anaanza kuomba baraka za wazazi na bibi mzaa baba ambao wamemlea kabla ya kufanya jambo.

Anasema hana kipingamizi kwenye muziki maana ni kipaji chake na anaendelea kumsaidia.

Maria anaeleza kuwa anachomwomba Mungu ni kusahau mkasa huo na kumfanikisha kijana huyo kuendeleza kipaji chake.



Msanii Rupia Boy. **PICHA: MTANDAO**

Anakumbusha kuwa walielekea Iringa pamoja na kufahamu alipopelekwa na kufanyiwa uganga huo, ambao anasema hakuuamini hata kidogo.

"Tuliambiwa atazikwa kwa muda. Nilishangaa mbona hakuna uhusiano? Utajiri na kuzikwa hai unahusianaje? Lakini tukazidi kujiuliza hayo ndiyo masharti mbona ni ajabu?"

Khamis ambaye wakati huo, alikuwa karibu zaidi na Rupia, hakumwacha aende Iringa peke yake aliambatana naye hadi porini na kushuhudia kilichoendelea akaazimia kuchukua hatua.

"Kwanza niliwaza kufukiwa ardhini kutasababisha kukosa hewa na kuzimia hata kupoteza maisha." Anasema Khamis ambaye sasa ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, akiwa kazini mkoani Tabora.

Anaeleza kuwa walimsaka mganga kwa simu kujua lini anamfukua, maana masharti hayo yalikuwa adhabu kwa ndugu yao, lakini hakupatikana kwa simu.

Anasema baada ya kuona wamepigwa changa la macho, walimfukua akiwa taabani asiyejitambua na kumkimbiza hospitalini.

"Huko nako tuliona kazi itakuwa ngumu maana mtu hajielewi, kusema alizikwa hai ingekuwa kesi nyingine. Hatuna fomu ya polisi namba tatu (PF3) hilo lilitatiza lakini tulikwenda kwenye hospitali binafsi kuomba huduma," anasema Khamis.

Anakumbuka kuwa wakiwa hospitalini walimfikisha kama jamaa ambaye wanakutana mitaani lakini safari hiyo hali yake ilishangaza marafiki zake wakalazimika kumfikisha hospitalini.

**ALIYEMWOKOA**

Huyu ni Ali Khamis, rafiki wa karibu wa Rupia, anayesema ilishindikana kumshawishi na kumkataza Salimu kukubalina na mganga.

Anasema wamekuwa pamoja na kusoma Sekondari ya Kileo na kwenye mpango wa kusaka hela chap chap, alimshauri aachane nao.

"Nilimshauri sikueleweka. Alikutana na watu wenye ushuhuda jinsi walivyofanikiwa na wakawa na nguvu kubwa ya ushawishi," anasema Khamis.

Anaeleza kuwa walikuwa pamoja hata alipoambiwa kuwa atazikwa hai, jambo lililomstua sana, akamkataza.

**ANA USHAURI**

Khamis anawataka vijana na yeyote anayetamani mafanikio afanye jitihada zaidi atumie mbinu bora na akili zaidi.

"Kupata maisha bora ghafla si rahisi. Ni kitu kigumu. Watu wakumbuke kuwa fedha au utajiri si mvua, jua au nguvu nyingine za asili. Tuongeze juhudi zaidi," anasema Khamis.

Aidha, anasema haiwezekani mtu wa kawaida akawa mfanyabiashara mkubwa ghafla akimiliki mfano mabasi ya mikoani bila kuanza na bodaboda, bajaji na daladala, akimaanisha kuwa ni lazima kupitia hatua ili kupanda juu zaidi.

"Jingine kubwa tusiamini na kupokea ushauri hasa wa watu ambao hatuwafahamu. Usikutane na mara moja na jamaa akakushauri ukamwamini. Hapana, akili au ushauri unaopewa changanya na wako."

Anaeleza kuwa watu waepuke kuamini shuhuda ambazo wakati mwingine si za kweli maana wengi wamepotelea au kuangamia kwa kupokea maelezo ambayo hayathibitishwi.

**KISA KILIVYOKUWA.**

Rupia akielezea mkasa huo uliochapishwa wiki iliyopita anasema, baada ya kufanya mawasiliano, alikutana na mganga huyo Sinza kwenye eneo la burudani.

Baada ya majadiliano na kulipa waliondoka Dar es Salaam kwenda Iringa kwenye msitu asioufahamu.

"Tuliondoka usiku mganga akiendesha gari lake binafsi. Tulifika sehemu hiyo akanionesha jeneza na kila kitu kilikuwa kimeandaliwa." Anasema Rupia.

Anaeleza kuwa, mganga alikuwa amewasiliana wa wenyeji wao na ilikuwa ni kufika na 'kutibiwa' au kufukiwa.

Anasema kabla ya kuingia kwenye jeneza la mbao, alichomwa sindano kwenye mshipa mkuu wa mkono wa kushoto, akapoteza fahamu.

Mganga alimwahidi kufukua baada ya siku mbili, na kwamba alifukiwa Ijumaa saa 9 usiku hivyo, angemfukua tena Jumapili saa 9 usiku pia.

Rupia, anasema aliingiwa na wasiwasi, katika safari hiyo aliyokuwa ameambatana na marafiki zake, akiwaambia, ikifika wakati huo kama mganga hajamfukua, wamfukue na iwapo atafariki au atapata shida yoyote wamwambie mama yake na hicho ndicho Ali Khamis alichokifanya.

SAYANSI

## NA MWANDISHI WETU

# Matajiri wanapojipeleka anga za mbali safari za kujirusha

Inatajwa kuwa ni safari hatari zaidi inayofanywa na mabilionea kutalii anga za mbali. Ikifanikishwa na chombo cha anga za juu cha kibinafsi Polaris Dawn, kilichoondoka duniani wiki iliyopita.

Kinaondokea Florida Marekani kikisaidiwa na roketi ya SpaceX Falcon 9, kikiwabeba bilionea Jared Isaacman, mwanzilishi mwenza wa kampuni ya malipo, Shift4, kwa mujibu wa BBC.

Pia yumo Scott "Kidd" Poteet, rubani mstaafu wa Jeshi la Anga la Marekani, na wahandisi wawili wa SpaceX, Anna Menon na Sarah Gillis.

Chombo hicho cha anga za juu, kiitwacho Resilience, kitaingia katika mzunguko wa kilomita 1,400 juu ya dunia.

Ikumbukwe hakuna binadamu aliyesafiri hadi sasa katika eneo hilo tangu mpango wa Apollo wa NASA ulipomalizika miaka ya 1970.

Wanaanga hao watapita katika eneo la anga za juu linalojulikana kama Van Allen Belt, lenye viwango vya juu vya mionzi, lakini watalindwa na chombo hicho chenye vifaa vyao vya kisasa vya anga za juu.

Kupita kwenye ukanda huo mara chache kutakuwa ni sawa na miezi na kupigwa na mionzi kwa miezi mitatu uzoefu walionao wanaanga kwenye Kituo cha Kimataifa cha Anga, ambacho kiko ndani ya mipaka inayokubalika.

Lengo la safari hiyo ni kujifunza madhara ya muda mfupi lakini salama ya mionzi kwa mwili wa binadamu.

Katika siku ya pili ya safari yao ya anga za juu wanaelezwa kuwa watafanya majaribio hadi 40, ikiwa ni pamoja na mawasiliano kati ya chombo cha anga za mbali cha Dragon na nyota ya setilaiti Space X.

**KUVUNJA REKODI**

Ikiwa mambo yote yatakwenda kama ilivyopangwa, siku ya tatu ya safari yao, Isaacman na Sarah Gillis wanatarajiwa kujaribu safari ya kwanza ya kibinafsi inayofadhiliwa, ambayo itadumu saa mbili angani.

Hii itafanyika wakati watakapokuwa kilomita 700 (maili 430) kwenye mzunguko, watajaribu mavazi mapya ya anga au suti za (EVA), ambazo, kama jina linavyoeleza, zimeboreshwa kulingana na shughuli za ndani za Space X (IVA) ili kufanya kazi nje ya chombo cha anga, wanaanga hao watakapohitaji kufanya shughuli hizo.

Mavazi yao yamebadilishwa kwa ajili ya kuhimili hali angani. Matangi ya ziada ya nitrojeni na oksijeni yamewekwa ndani ya chombo hicho na wanaanga wanne wanavaa mavazi mapya ya EVA, ingawa ni wawili watakaotoka nje ya chombo hicho kwa ajili ya kufanya uchunguzi.

Kwa hivyo ujumbe huo wa wanaanga utavunja rekodi



Wanaanga na mabilionea walioko safarini anga za juu; kutoka kushoto ni Anna Menon, Scott Poteet, Jared Isaacman na Sarah Gilli. **PICHA: MTANDAO**

ya idadi kubwa ya watu kuwahi kufika katika eneo lenye uwazi (vaccum) la anga za juu kwa wakati mmoja.

Wanaanga hao watafanya vipimo juu ya athari za ugonjwa wa decompression (matatizo yanayoweza kutokea kutokana na mgandamizo wa hewa), pamoja na hali ya wanaanga kushindwa kuona vizuri.

Jambo ambalo wakati mwingine huwapata wanapokuwa anga za juu, hali inayojulikana kama 'neuro-ocular syndrome'.

**VAZI JIPYA**

Vazi la EVA linajumuisha kofia ambayo hutoa habari za sauti wakati liponavaliwa ni rahisi kuvaliwa wakati wa kuondoka na kutua duniani na kuondoa hitaji la vazi jingine.

Katika mahojiano yaliyofanyika wakati wa mafunzo kwa ajili ya safari ya anga za juu, Gillis anaelezea kuwa vazi hilo ni sehemu muhimu ya mipango ya Space X ya kupeleka watu kwenye sayari nyingine.

"Hadi sasa, ni safari za kitaifa tu ambazo zimefikisha watu anga za juu. Space X ina matarajio ya kufika katika sayari ya Mars na kufanya maisha kuwa tofauti.

Ili kufanikisha hilo, tunapaswa kuanzia mahali fulani. Na hatua ya kwanza ni kujaribu mwingiliano wa kwanza na nafasi ya EVA ili tuweze kuboresha zaidi nafasi na miundo ya suti ya baadaye."

**HATARI KUBWA**

"Kuna hisia kuwa kuna hatari nyingi zinazohusika," Dk. Adam Baker, mtaalamu wa roketi katika Chuo Kikuu cha Cranfield cha Uingereza, alifafanua.

"Wamejiwekea malengo mengi ya kutamani na matamanio mengi huku chombo chenyewe kikiwa ni kidogo . Kwa upande mwingine, wametumia saa elfu kadhaa kuinigia kwenye eneo linalolengwa. Kwa hivyo wanafanya kila wawezalo kupunguza hatari," mtaalamu huyo anasema.

Ikiwa safari hiyo itafanikiwa, baadhi ya wachambuzi wanaamini kuwa itachochea kufanyika kwa safari nyingine binafsi zenye gharama ya chini ambapo watu wengi wataweza kusafirishwa zaidi kuliko mashirika ya anga za juu ya serikali ambayo yamewahi kufanya hivyo.

Lakini Beker ana mawazo tofauti: "Mpaka sasa sekta binafsi imetumia fedha nyingi, imefanya matangazo mengi, lakini idadi ya watu ambao wamesafiri kwenda anga za juu na kurudi imekuwa chini ya 100."

"Safari ya anga za juu ni ngumu, ghali na hatari, kwa hivyo kutarajia kuona idadi kubwa ya raia matajiri wanaoruka angani wakati wowote hivi karibuni, au kuwa miongoni mwao, haiwezekani." Anaiambia BBC.

**ANGA NA MATAJIRI**

Kwa wengine, wazo la mabilionea kujilipia kwenda anga za juu ni la kusikitisha, na linaibua maswali mengi.

Simeon Barber, mwanasayansi wa anga za juu katika Chuo Kikuu Huria nchini Uingereza ambaye anatengeneza vyombo vya kisayansi kwa ajili ya anga za juu katika miradi inayofadhiliwa na serikali pekee, anasema sio jambo la ubatili.

"Isaacman ni mwanaanga mwenye uzoefu zaidi ni yeye pekee amekuwa angani hapo awali, kwenye safari nyingine inayofadhiliwa na SpaceX, ambapo pia aliwahi kuwa kamanda. Katika muktadha wa ujumbe huo,ni chaguo la asili," anakaririwa.

Anasema wengi katika sekta ya anga za juu wanaamini kuwa ushiriki wa watu matajiri ni jambo jema.

"Kama wanataka kujitosa kwenye mtandao, na siku moja kwenda mwezini au hata Mars, itatengeneza fursa za kisayansi. Na sababu tofauti zaidi za kuchunguza anga za juu, mpango huo utakuwa na nguvu na manufaa zaidi."

## MAREKEBISHO SHERIA RUSHWA YA NGONO KUMBANA MWATHIRIKA, NAYE MTUHUMIWA

**INATOKA UK.11**

kutoka kona zote, waandishi wa habari, wadau wa kimataifa waliotuunga mkono," anasema Profesa Penina.

Anafafanua kuwa kwa kusimama kidete kupaza sauti zao na kukataa mapendekezo ya kifungu 10 (b) kilichotaka mwathirika wa rushwa ya ngono ashtakiwe kama mhalifu, kumeleta mafanikio katika jitihada za kuongeza utu wa mwanamke.

Mwenyekiti huyo anafafanua kuwa, bunge kuridhia kutopitisha kifungu hicho na kuongeza adhabu kwa waomba rushwa ya ngono, ni ushindi mkubwa kwenye mapambano dhidi ya unyanyasaji kijinsia.

Aidha, anasema ni uthibitisho tosha wa nguvu ya wananchi na umuhimu wa sauti za wanamtandao kama wanajamii katika kukataa mifumo kandamizi imezaa matunda.

Aidha, anasema kamati ya utawala, katiba na sheria imetimiza wajibu wake na kuishauri serikali kutopitisha kifungu hicho.

**MAREKEBISHO**

Bunge linaelezwa kuwa adhabu ya faini isiyopungua Sh. milioni mbili na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka mitano imewekwa katika makosa ya rushwa ya ngono.

Ni kwenye muswada wa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2024.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, anasema bungeni kuwa kifungu cha 25 kinaweka masharti kwa mwenye mamlaka.

Kinatamka kuwa ni kosa kwa mwenye mamlaka kuomba rushwa ya ngono au upendeleo wa aina nyingine kama sharti la kutoa au kupata ajira, cheo au haki.Katika ufafanuzi wake, anasema kifungu hicho kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu anayeahidi au kutoa rushwa ya ngono au upendeleo mwingine kwa mwenye mamlaka.

Kwa mwenye mamlaka au aliye katika nafasi ya mamlaka ili kumshawishi mtu huyo kutoa upendeleo wa ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

Aidha, muswada wa marekebisho ya sheria hii umependekeza kuongeza kosa na adhabu ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani.

"Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria nayo inapigilia msumari kuwa, wadau wengi wamelalamikia kifungu cha 10 (b) kwa kuwa kinawanyima waathirika wa rushwa ya ngono haki zao stahiki na kinawapa kinga wahusika wa vitendo hivyo." Anasema.



# Msako wauzaji mafuta kwenye vidumu, chupa waja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kuanza ukaguzi kwenye vituo vya mafuta, ili kubaini vinavyokiuka sheria kwa kuuza petroli kwenye vifaa visivyoruhusiwa ikiwamo madumu na chupa za plastiki.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dk. James Andilile, alitoa kauli hiyo jana kwa umma kutokana na hivi karibuni kukithiri kwa matukio ya milipuko ya moto inayotokana na kuhifadhi ama kuuza mafuta ya petroli kwa kutumia madumu na chupa za plastiki, kinyume na tahadhari ya usalama wa afya, mali na mazingira.

Alisema kwa mujibu wa kanuni namba 27 ya kanuni zinazosimamia biashara ya vituo vya mafuta za mwaka 2022 kama ilivyochapishwa katika Gazeti la Serikali Namba 150, wamiliki wote wa vituo vya mafuta wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kuhakikisha kuwa usalama wa afya, mali na mazingira unazingatiwa ili kuepusha milipuko ya moto.

**"Hivyo basi, mamlaka inawakumbusha wamiliki wote wa vituo vya mafuta kuzingitia matakwa ya Kanuni Namba 27 kwa kutoruhusu uuzwaji wa mafuta ya petroli kwenye**

"Hivyo basi, mamlaka inawakumbusha wamiliki wote wa vituo vya mafuta kuzingitia matakwa ya Kanuni Namba 27 kwa kutoruhusu uuzwaji wa mafuta ya petroli kwenye vifaa visivyoruhusiwa kuchukulia/kuhifadhia mafuta kama vile madumu, chupa za aina zote na vifaa vingine visivyoruhusiwa kisheria," alisema.

Aidha, alisema EWURA inatoa tahadhari kwamba maofisa wake watafanya ukaguzi ili kubaini kama kanuni hiyo inazingatiwa ipasavyo na atakayebainika kukiuka atachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria, ikiwamo kukifungia kituo husika.

Alisema: "Uuzaji mafuta kwenye vidumu na maeneo yasiyo rasmi unaweza kusababisha majanga ambayo yanagharimu maisha ya watu wengi hivyo nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kuacha tabia hii ni hatari sana kwetu na kwa wale wanaotuzunguka."



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akisalimia wahitimu wa darasa la saba na wananchi waliofika kwenye mahafali ya 60 ya Shule ya Msingi Kaloleni, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi watuma salamu kwa wagombea watoa rushwa

**Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANANCHI wa Mkoa wa Singida wamesema wamejipanga katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu hawatawachagua wagombea wanaotoa rushwa ili wapate uongozi.

Walisema hayo juzi kwenye banda la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yaliyohitimishwa mwishoni mwa wiki mjini hapa.

Walisema elimu iliyotolewa na taasisi hiyo imewasaidia kubaini viashiria vya rushwa na kwamba wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wagombea wasifanye fedha kama ndiyo sifa ya kutaka kuchaguliwa.

Mmoja wa wananchi hao Rajabu Nkangu, alisema TAKUKURU imefanya kazi nzuri kuwaelimisha madhara ya rushwa, hivyo wagombea ambao kila inapofika wakati wa uchaguzi wanatumia pesa kuwahonga wananchi ili wawachague sasa wajipange hawadanganyika tena.

"Wakati wa uchaguzi baadhi ya wagombea wanatumia pesa zao kutuhonga ili tuwachague na viongozi wa namna hii wakishachaguliwa wanakaa mbali na sisi bila kuleta maendeleo yoyote, sasa tumeamka wenye tabia hiyo bora wasije kuchukua fomu hatutawachagua," alisema.

Naye Godfrey Gunda alisema elimu waliyopewa na TAKUKURU itawasaidia sana wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika Novemba mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani ambapo wataitumia kama fimbo ya kuwaadhibu wagombea watoa rushwa.

Gunda alisema kuchagua kiongozi mtoa rushwa wamebaini kumekuwa kukiwagharimu sana kutokana na kukaa miaka mitano bila kuletewa maendeleo kwasababu viongozi wanaotoa rushwa wakishachaguliwa wanakuwa hawana muda wa kuwatumikia wananchi.

Amina Selemani alisema atakuwa balozi kwa wananchi wengine kuwaelimisha madhara yatokanayo na rushwa kwani rushwa inazorotesha maendeleo ya nchi na kuwafanya wananchi kukosa haki za msingi.

Kwa upande wake Naibu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Petro Horombe, alisema katika kipindi cha wiki moja ya maonesho hayo banda lao lilitembelewa na wananchi wengi wakiwa viongozi wa vyama vya siasa na watendaji wa serikali.

"Wananchi wasiopungua 115 wamefika kwenye banda letu ambapo wote waliofika wamenufaika kupata elimu juu ya mapambano dhidi ya rushwa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani," alisema Horombe.

Horombe alisema TAKUKURU ilichobaini kwenye maonesho hayo kwa wananchi waliofika katika banda lao wameipenda elimu waliyopewa, wameipokea na wamekubali kutoa ushirikiano kwa taasisi katika kukomesha vitendo vya rushwa nchini.

"Wananchi waliofika katika banda la TAKUKURU tafsiri yake kila mmoja akiwa balozi wa mwenzake akimwelimisha ndugu yake, jirani yake, mtoto wake, mke wake, mume wake na kadhalika maana yake elimu hii itasambaa sana," alisema.

Horombe alisema elimu waliyoitoa ni ya msingi kwani ni sehemu ya uzuiaji rushwa na wananchi wanapokuwa wameelimika juu ya madhara ya rushwa watajua thamani ya kura wanayopiga wakati wa uchaguzi.

# BAKWATA yalaani matukio ya utekaji na mauaji

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limesema kuwa vitendo vinavyojitokeza vya ubakaji, utekaji na mauaji vinaweza kuwasababishia Watanzania kurudi nyuma kiuchumi, kutokana na hofu waliyokuwanayo hivi sasa ya kukosa amani.

Kauli hiyo imetolewa na Kaimu Shekhe wa Wilaya ya Dodoma, Abdallah Msafiri alipokuwa akizungumza na mashekhe, maimamu, walimu na viongozi wa idara ya wanawake na vijana ngazi ya wilaya na kata kwenye kikao cha utambulisho wa viongozi wapya wateule wa Mufti wa ngazi mbalimbali za uongozi ndani ya BAKWATA.

Shekhe Msafiri, alisema kuwa kutokana na hali hiyo Bakwata wanakemea na kulaani vitendo hivyo viovu vya udhalilishaji vinavyojitokeza katika maeneo mbalimbali kwa kuwa hivi sasa Watanzania hawafanyi kazi zao za uzalishaji kwa amani na uhuru bali wamekuwa wakifanya kwa hofu.

Hivyo, aliwaomba viongozi wa dini ya kiislamu wa ngazi mbalimbali wakiwamo mashekhe, kuhakikisha wanakemea kwa nguvu kwa kuhubiri kupitia nyumba zao za ibada, ili kwa wale wanaojihusisha waweze kujiepusha na tabia hiyo na wawe na hofu ya Mungu.

Alisema pamoja na kujitokeza kwa vitendo hivyo Watanzania pia waamini kuwa serikali kwa upande wake kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama itahakikisha kuwa inakomesha tabia hiyo na hali ya utulivu itakuwapo.

Naye Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashiru Omary, aliwakumbusha viongozi wa dini kutumia misikiti yao kuwataka watu kumrudia Mungu ili waepukane na vishawishi vinavyosababisha kujihusisha na vitendo vya utekaji, mauaji na ubakaji.

Alisema kwa kutumia nafasi zao kama viongozi wanauweza mkubwa wa kuwashawishi watu kutojiingiza kwenye vitendo hivyo vya kikatili ambavyo ni laana mbele za Mungu na hatimaye wakawa wema tu. Pia aliwataka viongozi walioteuliwa katika nafasi mbalimbali za BAKWATA wakiwamo mashekhe, maimamu na idara kufanya kazi zao za maamuzi kwa haki na uwazi.

Alisema: "Kwenye uteuzi wenu kuna walioteuliwa kushika nafasi za ukadhii wa mahakama na wengine mashekhe, wote nyinyi mnakutana na kesi za kutatua changamoto za ndoa na zinginezo, hivyo mnapotoa hukumu mtende haki bila kuangalia mwenye kipato kikubwa".



# Ukivamiwa na nyuki ziba mdomo, masikio na macho

**Na Mwandishi Wetu,**
MAFINGA

BAADA ya kukithiri kwa matukio ya wananchi kushambuliwa na makundi ya nyuki katika maeneo mbalimbali nchini, wadau wa maendeleo wameanza kutoa elimu kwa wananchi namna ya kuepuka madhara ya wadudu hao.

Shirika la Maendeleo Vijijini (RDO), ndilo limejitosa kutoa elimu kwa wananchi ambapo limewataka wananchi kujikinga kwa kuziba midomo, masikio na macho, pale wanapokutana na kundi la nyuki.

Akizungumza na waandishi wa habari wilayani Mafinga mkoani Iringa, Ofisa Nyuki RDO, Teddy Pagi alisema binadamu aking'atwa na nyuki kwenye maeneo hayo ya wazi huwa ni rahisi kupoteza maisha.

Alisema nyuki huwa wanachagua sehemu hizo muhimu kwa binadamu kuuma na kwamba sehemu hizo zikivimba ni rahisi binadamu kupoteza maisha kwa maelezo kuwa zikivimba inamuwia vigumu binadamu kupumua.

Kutokana na hilo alisema watu wanapaswa kuwa makini na siyo kukimbia peke yake bila kuwa na tahadhari yoyote ile kwenye viungo vya mwili wake.

**Mbali na madhara ya nyuki pia alizitaja baadhi ya faida zitokanazo na mazao ya nyuki ikiwamo asali na maziwa ambavyo vinatumika kama chakula na dawa pamoja na sumu...**

Mbali na madhara ya nyuki pia alizitaja baadhi ya faida zitokanazo na mazao ya nyuki ikiwamo asali na maziwa ambavyo vinatumika kama chakula na dawa pamoja na sumu ambayo hutumika kama malighafi.

Alisema asali inatumika kama tiba katika matatizo mbalimbali ambazo binadamu anakutana nazo ikiwamo kuungua moto katika baadhi ya sehemu za mwili.

Alisema sumu ya nyuki inatumika kama kinga ya kuimarisha viungo vya mwanadamu yeyote yule isipokuwa sehemu ya ulimi, pua macho na masikio.

Hivyo, aliishauri jamii kufuga nyuki kwa wingi ili wavune mazao yake ambayo yatawapa faida wao na familia zao.

Pia alitoa ushauri kwa wafugaji wa nyuki kuhahakikisha wanatumia mizinga mizuri ambayo nyuki watatengeneza asali itakayowapa manufaa.

Alisema lengo lao ni kuona jamii inafaidika na mazao ya nyuki na siyo kuwakimbia badala yake wafuge ili wapate faida kupitia mazao yanayotolewa na nyuki.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (kulia), akibadilishana maazimio ya kongamano la kisayansi la pili na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afrika Mashariki, Abdi Dubat, kwenye kilele cha maadhimisho ya 13 ya Siku ya Mara, yaliyofanyika Narok, Kenya juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tamasha kuenzi mila, desturi za makabila kufanyika

**Na Mwandishi Wetu,**
RUVUMA

TAMASHA la kitaifa la utamaduni linatarajiwa kufanyika mkoani Ruvuma kwa siku nne, lengo likiwa ni kuenzi mila, desturi na tamaduni za makabila mbalimbali ya Tanzania.

Ufunguzi wa tamasha hilo ambalo ni la tatu la Mkoa wa Ruvuma unatarajiwa kufanyika Septemba 20, mwaka huu na kuhitimishwa Septemba 23.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Ahamedi Abas Ahamedi, alisema kuwa tamasha hilo litafunguliwa na Waziri wa Michezo, Sanaa na Utamaduni, Dk. Damas Ndumbaro na kwamba litafungwa Septemba 23 na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema tamasha hilo linasaidia katika kuimarisha utalii wa kiutamaduni nchini na watalii kutoka mataifa mbalimbali huvutiwa na utajiri wa kitamaduni wa Tanzania, hivyo tamasha hili linakuwa kivutio kwao.

Alisema utalii wa kiutamaduni unachangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya nchi na tamasha hili limekuwa na mchango mkubwa katika sekta hiyo.

Tito Mbilinyi maarufu kama Mwilamu alisema wageni kutoka katika mikoa mbalimbali nchini watakaokwenda mkoani humo watasaidia kuwainua kiuchumi wananchi wa eneo hilo kutokana na kununua bidhaa na huduma mbalimbali zinazotolewa.

Upendo Hosia ambaye ni mfanyabiashara mkoani humo, alisema taarifa ya ujio wa Rais Samia wamezipokea kwa furaha na watahakikisha wanatumia fursa hiyo kuuwezesha mkoa huo unanufaika kiuchumi.

Alisema uchumi wa mkoa huo umekuwa ukiimarika siku hadi siku kutokana na kupita magari makubwa ya mizigo yanayochukua shehena ya mizigo kusafirisha maeneo mbalimbali.

# Barabara Mtili-Ifwagi-Mkuta kuchochea ukuaji biashara

**Na Renatha Msungu,**
MUFINDI

UJENZI wa Barabara ya Mtili-Ifwagi hadi Mkuta katika Wilaya ya Mufindi mkoani Njombe kiwango cha lami utasaidia kuchochea ukuaji wa biashara za wananchi wa maeneo hayo.

Mbunge wa Mufindi Kaskazini, Exaud Kigahe ambaye ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara alisema hayo juzi wakati akikagua barabara hiyo.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo unaendelea ambapo upo katika hatua za mwisho kuanza kuwekwa lami na inaunganisha vijiji vya Mtili, Ifwagi na Mkuta.

Alisema barabara hiyo ikikamilika itazidi kupanua wigo wa kiuchumi kwa wakazi wa vijiji vilivyoko ndani ya wilaya hiyo hasa vya pembezoni mwa mji.

Kigahe alisema lengo lake ni kuona barabara hiyo inakamilika kwa wakati ili wakulima na wafanyabiashara waitumie kujiinua kiuchumi.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni awamu ya kwanza na kwamba baadaye wataanza awamu ya pili kutoka Mkuta, Mdabulo mpaka Kata ya Ihemi.

Alisema kutokana na umuhimu wa barabara hiyo kwa wananchi ndiyo sababu alikwenda jimboni humo kwa ajili ya kuhakikisha wanasimamia miundombinu hiyo kuimarika kama serikali inavyoelekeza.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ukikamilika wananchi wa eneo hilo watanufaika na matumizi ya miundombinu hiyo.

Hivyo, aliwataka wakazi wa jimbo lake kuendelea kutoa ushirikiano kwa serikali pale wanapohitajika, ikiwamo kutunza miundombinu inayojengwa na serikali.

# Washauri faini ya 50,000/- wanaotumikisha watoto

**Na Elizabeth John,** MAKETE

VIONGOZI wa Serikali ya Kijiji cha Ndulamo wilayani Makete mkoani Njombe, wameshauriwa kuweka faini ya shilingi 50,000 kama adhabu kwa mtu atakayebainika kutumikisha watoto wadogo kwenye biashara ya kubeba mbao.

Ushauri huo, ulitolewa juzi na Mjumbe wa Baraza Kuu la Chama Cha Mapinduzi CCM Taifa Mkoa wa Njombe, Rabison Mahenge katika mahafali ya darasa la saba Shule ya Msingi Ndulamo.

Alisema uwepo wa sheria hiyo utasaidia kukomesha tabia ya watoto kwenda kubebeshwa mbao badala ya kwenda shule.

Mahenge alisema wananchi wa kijiji hicho wasiwe watu wa kupigia makofi na kusifia watu kuendelea kutumikisha watoto badala yake wawe mfano bora wa kukemea ili kuwa na wasomi wengi.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ndulamo, Mariam Charahani, alisema ni kweli wazazi na walezi wana tabia ya kuwatumikisha watoto katika vibarua vya kubeba mbao hali inayosababisha kukosa masomo.

Ofisa Elimu Kata ya Iwawa, Naumu Tweve alisema wazazi wanapaswa kutambua kwamba wanao wajibu wa kuisaidia serikali kupata watumishi na wasomi kutoka kijiji hicho.

Mmoja wa wakazi wilayani Makete, Fanuru Mahenge, alikiri kwamba kweli wazazi wengi wamekuwa hawaoni umuhimu wa watoto wao kuendelea na masomo jambo ambalo ni hatari kwa maisha ya baadaye.

HABARI ZANZIBAR

# Matukio utapeli wa viwanja yakithiri Unguja, Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imesema bado vitendo vya udanganyifu vinaendelea kujitokeza kwa wingi vya ukataji wa maeneo ya ardhi na kuuza viwanja katika maeneo ya Unguja na Pemba.

Akizungumza na wandishi wa habari ofisini kwake, Waziri wa Wizara hiyo, Rahma Kassim Ali, alisema wauzaji hao hutumia matangazo kwa njia tofauti ikiwamo mitandao ya kijamii, ambayo huwahamasisha wananchi kununua viwanja vya makazi na biashara katika maeneo hayo.

"Tunapenda kuwafahamisha wananchi wote kuwa vitendo hivyo ni kinyume na taratibu za kisheria kwa kuwa Kamisheni ya Ardhi haihusishwi na haitambui upangaji, upimaji na ukataji wa viwanja hivyo," alisema.

Alisema Kamisheni ya Ardhi ndiyo chombo pekee chenye mamlaka na jukumu la kupanga na kusimamia mpango wa kitaifa wa matumizi ya ardhi katika maeneo yote ya Zanzibar.

Alisema upangaji wa maeneo ni taaluma mahsusi na siyo kila mtu anaweza kupanga na kupima miji au vijiji, kwamba yapo mambo mengi yanapaswa kuzingatiwa katika upangaji wa maeneo ya ardhi.

Aidha, alisema maeneo hayo yanayokatazwa na kuuzwa hayazingatii uweledi wa upangaji wa maeneo na kusababisha kuharibu haiba ya miji na vijiji na kuathiri mipango ya serikali ya kufikisha huduma za kijamii kwa wananchi.

Hivyo, aliwatahadharisha wananchi kuwa vitendo hivyo ni kinyume na masharti ya kifungu cha 6B cha Sheria ya Matumizi ya Ardhi kinachozuwia mtu yeyote kuitumia vibaya ardhi kwa kubadilisha matumizi ya ardhi hiyo au kwa kutumia kinyume na utaratibu uliowekwa kisheria.

"Kwa mujibu wa kifungu hicho, atakayetiwa hatiani kwa makosa hayo atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi 500,000 na isiyozidi shilingi 200,000 au kutumikia kifungo jela kwa kipindi cha miezi sita au vyote kwa pamoja," alisema.

Alisema baadhi ya viwanja vinavyokatwa na kuuzwa imebainika kuwa vimeingia katika maeneo ya serikali kama vile maeneo ya misitu, hifadhi ya serikali maeneo yaliokaribu na fukwe.

Alisema maeneo hayo hayaruhusiwi kuuzwa na itakapobainika yatarejeshwa serikalini.

Alisema wizara yake kupitia Kamisheni ya Ardhi inaendelea kufuatilia uhalali wa umiliki wa maeneo hayo kabla ya kuchukuwa hatua stahiki.

Hivyo aliwataka wananchi kujiepusha na ununuzi wa viwanja hivyo ili kutojiingiza katika hasara.

# Daktari ataja mbinu kuepuka magonjwa yasiyoambukiza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Jumuiya ya Magonjwa Yasioambukiza Zanzibar, Dk. Omar Abdallah Ali, amesema ni vyema jamii kuwa na utamaduni wa kula chakula bora ili kuepukana na athari za maradhi yasiyoambukiza.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupunguza kasi ya wagonjwa wa maradhi ya kuambukiza ambapo sasa ni tishio kutokana na wagonjwa na vifo vingi vitokanavyo na maradhi yasioambukiza.

Alitoa kauli hiyo wakati akiwasilisha mada kuhusu athari za maradhi yasioambukiza katika mafunzo ya kuwajengea uwelewa waandishi wa habari na wasanii visiwani humo, ili kuwa mabalozi wazuri kwa jamii kuhusu kujikinga na magonjwa hayo.

Aliyataja baadhi ya maradhi hayo ni kisukari, shinikizo la damu, saratani ambayo ndiyo tishio kubwa na yanatokana na viashiria mbalimbali ikiwamo mlo usiosahihi, kutofanya mazoezi, utumiaji wa vyakula vyenye kemikali na matumizi ya vileo ikiwamo pombe, sigara, shisha na tumbaku.

Alisema miongoni mwa changamoto kubwa iliopo hivi sasa nchini ni kukitihiri kwa maradhi hayo na husababisha vifo vya watu wengi, kwamba asilimia 74 ya vifo duniani vinatokana na maradhi yasioambukiza.

**Alisema ugonjwa wa kiharusi ambao husababishwa na shinikizo la damu ndiyo unaongoza kwa idadi ya vifo duniani, hivyo juhudi za makusudi zinahitajika katika kupambana na magonjwa...**

Alisema ugonjwa wa kiharusi ambao husababishwa na shinikizo la damu ndiyo unaongoza kwa idadi ya vifo duniani, hivyo juhudi za makusudi zinahitajika katika kupambana na magonjwa hayo.

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Muungano wa Jumuiya ya Maradhi yasioambukiza Zanzibar (Z-NCDA), Dk. Said Gharibu Bilali alisema maradhi hayo yamekuwa yakiathiri jamii.

Alisema hatua hiyo ya kutoa elimu kwa waandishi wa habari na wasanii itasaidia kuongeza uelewa na kujikinga nayo.

Dk. Said alisema maradhi yasiyoambukiza yameshika kasi kubwa ndani ya jamii, hivyo ni vyema kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maradhi hayo ili jamii kujikinga na kuwa salama.

"Maradhi yasioambukiza yanaongezeka siku hadi siku na kusababisha kuzuia maendeleo ya mtu mmoja mmoja na ukuaji wa familia, hivyo ni vyema kutumia nafasi zenu katika kuielimisha jamii ili kujikinga na maradhi hayo," alisema Dk. Bilali.

Meneja wa Jumuiya hiyo Zanzibar, Haji Khamis Fundi, aliitaka jamii hasa wanaume kuwa na utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara kwa sababu uzoefu unaonesha kuwa wanaume ni wagumu zaidi kuangalia afya zao ikilinganishwa na wanawake.

Aidha, aliwataka wagonjwa wa maradhi yasioambukiza kufuata maelekezo ya watalamu wa afya ili kupunguza athari za magonjwa hayo na kuachana na dhana potofu kuhusu magonjwa hayo.

Alisema kuna baadhi ya wagonjwa wanaosumbuliwa na maradhi hayo wanaimani za kishirikika na badala ya kwenda hospitali kupata tiba sahihi wanakimbilia kwa waganga wa kienyeji wakiamini ni masuala ya ushirikina.




Baadhi ya wananchi waliojitokeza kupata matibabu ya huduma za afya katika kambi maalum ya matibabu ya afya ya macho katika Shule ya Uweleni Pemba, matibabu hayo yanatolewa bure na Taasisi ya Bilali Muslim Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Tigo Zanteli. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ripoti kuhusu usalama wa mazingira, jamii yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

RIPOTI ya mazingira, jamii na utawala (ESG) imezinduliwa ambayo imeangazia masuala ya mazingira na jamii kwa Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi huo, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya CSI Energy Group, Natacha Emilian, alisema lengo lao ni kuhakikisha Bara la Afrika linakuwa la kijani kibichi. Alisema masuala yaliyomo katika ripoti hiyo yanadhihirishwa kupitia miradi kama vile Kinyerezi 1 hapa nchini, mtambo wa kuzalisha umeme wa gesi asilia ambao umeimarisha usalama wa nishati nchini, kuokoa Dola za Marekani milioni 500 za gharama za mafuta na kutoa nishati kwa zaidi ya Watanzania milioni moja.

Kuhusu jamii, alisema wamefanikiwa kutengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo rasmi kwa ajili ya wakazi wa eneo husika.

Alisema kwa mwaka jana CSI ambayo imejikita katika masuala ya nishati ilitoa nafasi za kazi zaidi ya 500, kwamba 85 zilikuwa za wanawake na wanafunzi 26 ambao walipewa nafasi za mafunzo kwa vitendo.

Naye Meneja Uendelevu wa CSI, Christine Nafula, alisema dhumuni ni kushirikiana na wachuuzi wa chakula nchini ambako kumechochea shughuli za kiuchumi na kuinua jamii.

Alisema katika masuala ya utunzaji wa mazingira CSI imepitisha mipango mbalimbali ikiwamo kupunguza uzalishaji wa kaboni kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2025.

# Wakazi Ngorongoro kupiga kura kwenye maeneo yao

**Na Allan Isack,** ARUSHA

'NIMESIKIA kilio chenu'. Ndivyo unavyoweza kueleza, baada ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kutafakari na kisha kurejesha takwa la kikatiba kwa wakazi wa Ngorongoro, mkoani Arusha na maeneo mengine nchini, kushiriki upigaji kura kwenye maeneo ya kiutawala ya vijiji 12,333 vilivyokuwa vimefutwa.

Hatua ya urejeshaji wa vijiji hivyo, inatokana na maeneo yaliyokuwa yamefutwa awali kwa mujibu wa Tangazo la Serikali, Namba 673 na 674, ambayo yalihusisha, pia Tarafa ya Ngorongoro inayokaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa jamii ya Kimasai.

Jana, Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, akizungumza jijini Arusha kuhusu amri na notisi (ilani) ya mgawanyo wa maeneo ya kiutawala katika serikali za mitaa, alisema mbali na maeneo ya vijiji hivyo kurejeshwa, pia kuna mitaa 4,269 na vitongoji 64,274 imerejeshwa kwenye maeneo ya kiutawala.

Aidha, alisema lengo la kuchukua hatua hiyo ni kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanapata uwakilishi mzuri wa kiutawala pamoja na huduma za kijamii na kiuchumi zinazowiana na mahitaji ya wananchi wake.

Alisema serikali itaendelea kutekeleza majukumu yake, kwa kuzingatia misingi ya kisheria na utawala bora, na kwa muktadha huo, tayari imetoa amri na notisi ya mgawanyo wa maeneo ya kiutawala katika Serikali za Mitaa.

"Amri ya mgawanyo wa maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) kutokana na tangazo la Serikali Na. 796 la mwaka 2024, imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287.

"Notisi (ilani) ya mgawanyo wa maeneo ya utawala katika Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) kutokana na tangazo la Serikali Namba 797 la mwaka 2024), imetolewa kwa mujibu wa vifungu vya 16 (1) na 18 (1) vya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

"Napenda kueleza kuwa amri na notisi hizi ndizo ambazo zimeainisha mitaa, vitongoji na vijiji vitakavyoshiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika tarehe 27 Novemba 2024," alisema Waziri Mchengerwa.

Pia, alisema uchaguzi huo ni muhimu kwa ustawi wa demokrasia ya nchi ya Tanzania na maendeleo ya Serikali za Mitaa.

"Naendelea kuwasisitiza wananchi umuhimu wa kujitokeza kwa wingi kwa wote wenye sifa, ili kushiriki kikamilifu katika kuunda serikali ya wananchi kidemokrasia.

"Ni muhimu kuhakikisha mnajiorodhesha katika orodha ya wapigakura itakapofika Oktoba 11 hadi 20, ambayo itatumika siku ya uchaguzi tarehe 27, pia tunawahimiza wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Serikali za Mitaa kuchukua hatua za mapema za kujiandaa na kushiriki kikamilifu," aliongeza Mchengerwa.

Wakati huo huo, Waziri Mchengerwa, alisema mchakato huo, ni fursa kwa wananchi kushiriki moja kwa moja kuamua mustakabali wa maendeleo ya maeneo yao.

Alisema uongozi imara katika ngazi ya mitaa, vitongoji na vijiji unahitajika ili kuendeleza juhudi za serikali za kujiletea maendeleo endelevu.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makondo, alimpongeza Waziri Mchengerwa kwa kazi nzuri anayofanya kwa kuwasimamia vema wakuu wa mikoa wote nchini.

"Maelekezo yote yanayotoka kwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan yanapita kwako na yanakuja moja kwa moja kwetu na mimi sina budi kukushukuru kwa kuwa kwa mara ya kwanza napata nafasi ya kukukaribisha Arusha tangu nilipokuwa Mkuu wa Mkoa," alisema Makonda.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Marekani Mohamed Bayo, alisema wamepokea tangazo hilo kwa furaha kwa kuwa vijiji 65 na vitongoji 242 wilayani humo, wananchi watashiriki katika uchaguzi na kupiga kura.



Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga, akizungumza mwishoni mwa wiki kuhusu ujenzi wa hosteli za chuo hicho kwa ubia. Kushoto ni Naibu Mkuu wa chuo, anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, Dk. Emmanuel Munishi na kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Mipango, Dk. Nina Buna. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# YST kutoa tuzo kwa wanafunzi gunduzi za kisayansi

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), inatarajia kutoa tuzo kwa wanafunzi ambao wamechaguliwa baada ya kuwa na gunduzi nzuri za kisayansi zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali kwenye jamii.

YST inatarajia kutoa tuzo kwa wanafunzi hao Septemba 19, mwaka huu, jijini Dar es Salaam kutoka katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Yunus Mgaya, alisema wanafunzi hao wamepatikana baada ya kufanyiwa mchujo ulioshirikisha kazi 1,055 kutoka kwa wanafunzi wa mikoa mbalimbali ya pande zote za Muungano.

"Idadi ya wanafunzi waliowasilisha maombi kuonyesha gunduzi zao mwaka huu ilikuwa kubwa, maombi 1,055 yalipokewa na kati ya hayo, wanafunzi wenye gunduzi 394 walishiriki katika mafunzo ya sayansi na mwisho wa mafunzo, gunduzi 191 zilitengenezwa na kukamilika na 45 zilizoonekana kuwa bora zaidi na zilichaguliwa kushiriki na kuonyeshwa katika maonesho ya kitaifa Septemba 19," alisema Prof. Mgaya.

Alisema gunduzi za mwaka huu, zimejikita katika masuala mbalimbali ikiwamo uhifadhi salama wa mazao ya kilimo, afya ya binadamu, mifumo ya umwagiliaji, utunzaji wa mazingira, upatikanaji wa nishati ya umeme, usalama wa chakula na utatuzi wa changamoto kidijitali.

Alisema jumla ya wanafunzi 90 na walimu 45 watapata fursa ya kushiriki na kuonesha kazi zao katika maonesho hayo ya kitaifa jijini Dar es Salaam.

Mwakilishi wa mdhamini mkuu wa maonesho hayo kwa miaka 14 mfululizo ya YST kutoka Karimjee Foundation, Caren Rowland, alisema wamekuwa wakitoa ufadhili huo ili kuwajengea uwezo na msingi thabiti wa elimu ya sayansi vijana wa Kitanzania ili kukuza ujuzi wao na kuwasaidia kuchangia katika maendeleo ya taifa lao.

"Kupitia ushirikiano huu Karimjee Foundation inajivunia kuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya sayansi nchini Tanzania. Ni fahari kuona mafanikio makubwa kwenye miradi ya kijamii tunayoisaidia ikiwamo huu wa YST, ambao umetoa jukwaa kwa wanasayansi chipukizi ambao wengi ni wanafunzi, kuimarisha elimu ya sayansi nchini," alisema Caren.

Alisema Karimjee Foundation inaamini kuwa uwekezaji katika sayansi ni njia bora ya kukuza ujuzi kwa vijana, kusaidia maendeleo ya jamii na taifa pamoja na kujenga mustakabali bora wa Tanzania.

"Kwa juhudi hizo, Foundation inathibitisha dhamira yake ya kuendelea kulea kizazi kijacho na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya elimu na uchumi wa Tanzania. Jitihada zinazofanywa na YST katika kuchochea ukuaji wa sayansi, ubunifu na teknolojia kwa vijana wa nchi hii ni mfano wa kuigwa kwa sababu inasaidia kukuza sayansi na kuongeza hamasa kwa wanasayansi kuimarisha zaidi ujuzi na maarifa," alisema Caren.

Alisema katika kila maonesho, Karimjee Foundation imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa washindi kila mwaka na mpaka sasa imewapatia ufadhili wa masomo wanafunzi 45 ambao wengine ni wa kuendelea na elimu ya juu na mwaka huu itaongeza ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wengine wanne watakaoshinda.

# Wananchi wajengewa kituo cha afya chenye umeme wa jua

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Kisiwa cha Rukuba, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Vijijini, mkoani Mara wameondokana na adha ya usafirishaji wa wagonjwa kwa boti baada ya serikali kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya kilichowekwa umeme jua (solar).

Kisiwa hicho, kilichotambuliwa na kupata hadhi ya kijiji mwaka 1974, awali wagonjwa walilazimika kutumia usafiri wa majini kufika kwenye huduma za upasuaji mdogo nje ya kisiwa hicho.

Kwa sasa, adha hiyo imetatuliwa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kusikia kilio cha wananchi na kwa kushirikiana na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, kufanikisha ujenzi wa kituo hicho kwa gharama ya Sh. milioni 500, pamoja na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 100.

Hassan Juma Ibrahim, mmoja wa wakazi wa Rukuba, aliishukuru serikali na mbunge kwa jitihada zao.

"Mbunge wetu amefanikisha kutuletea mradi wa REA wa shilingi 345 kwa ajili ya umeme jua, ambao utawezesha wagonjwa kupata huduma za matibabu nyakati za usiku bila shida yoyote."

Abdallah Suma, alisema kuwa awali walikuwa wakikabiliwa na ugumu ikiwa mama anahitaji upasuaji mdogo wa dharura, lakini sasa umeme jua utamaliza tatizo hilo. "Umeme jua huu sio tu utasaidia sekta ya afya bali pia elimu, hivyo namshukuru Rais Samia na mbunge wetu," alisema Suma.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Musoma, Thomas Kipango, alisema kituo hicho kimeondoa ugumu wa kusafirisha wagonjwa kwa njia ya maji kwa kutumia boti, ambapo walikuwa wakitumia zaidi ya saa moja na nusu kufika kwenye huduma za matibabu nje ya kisiwa hicho.

Kisiwa cha Rukuba, ambacho kinategemea uvuvi kama njia kuu ya uchumi ni moja ya vijiji vinne vya Kata ya Etaro, ikiwa ni pamoja na Busamba, Etaro na Mmahare.

# Ruto ajipambanua mikakati ya serikali anayoiongoza

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, ametetea rekodi yake ya miaka miwili madarakani akisema hakuna serikali ya nchi hiyo iliyowahi kuweka mikakati madhubuti ya kuiendeleza Kenya kuliko ile anayoiongoza.

Rais Ruto ameyasema hayo kwenye mahojiano maalumu aliyofanyiwa na DW mjini Berlin wakati alipofanya ziara ya siku mbili nchini Ujerumani wiki iliyopita.

Ruto alikuwa mjini Berlin kushiriki Tamasha la Wananchi wa Ujerumani ´BürgerFest´ ambalo huandaliwa kila mwaka na Ofisi ya Rais wa Ujerumani, pamoja na kutia saini mkataba utaowezesha maelfu ya Wakenya wenye ujuzi kupata nafasi za kazi nchini Ujerumani.

Akizungumzia malalamiko ya umma juu ya gharama kubwa za maisha na ukosefu wa ajira, Ruto alisema rekodi ya serikali yake haina mpinzani, akijinadi kwamba tangu alipoingia madarakani ameweka mikakati ya makusudi ya kushughulikia changamoto zinazolikabili taifa hilo.

"Hakuna serikali nyingine iliyowahi kuwa na mpango kama niliokuwa nao mimi. Wa kwanza ni ujenzi wa makazi ya gharama nafuu tayari umetengeneza nafasi za ajira 160,000 ... nafasi za kazi zitokanazo na teknolojia ya dijitali ni 140,000," alisema Rais Ruto.

Aliongeza kuwa mkataba alioutia saini Jumamosi iliyopita na Kansela Olaf Scholz wa Ujerumani utaongeza nafasi za kazi kwa vijana wa Kenya.

Kulingana na kiongozi huyo, mkataba huo utawawezesha wafanyakazi wenye ujuzi mkubwa na wa kati kupata nafasi za ajira nchini Ujerumani. Huku akizitaja baadhi ya kada zitakazonufaika kuwa ni pamoja na sekta ya afya, elimu na fani za uhandisi na ufundi.

Akijibu hoja za baadhi ya wanasiasa na vijana wa Kenya wanaoukosoa mpango huo, Rais Ruto alisema, „Hakuna kijana Mkenya ambaye atalazimishwa kwenda mahala popote. Wale ambao tutawasaidia kupata nafasi ya ajira Kenya, hilo litakuwa chaguo letu la kwanza, lakini hatutawazuia wale ambao azma yao ni kufanya kazi nje ya Kenya."

Baadhi ya wanasiasa na wananchi waliitumia mitandao ya kijamii mwishoni mwa juma kukosoa uamuzi wa serikali ya Rais Ruto wa kutia saini mkataba huo wakisema jukumu la serikali ni kutengeneza fursa za ajira ndani ya nchi hiyo badala ya kutafuta fursa hizo kwenye mataifa ya kigeni.

Kiongozi huyo alisema pamoja na juhudi ambazo serikali yake inachukua, itakuwa vigumu kumaliza tatizo la ukosefu wa ajira nchini Kenya na ndiyo maana mikataba kama ule aliotia saini na Ujerumani ni muhimu.

Takwimu za nchi hiyo zinaonesha zaidi ya vijana wenye ujuzi milioni 1 huingia kwenye soko la ajira kila mwaka, kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na uwezo wa uchumi wake.

Takwimu za Taasisi ya Statista ya nchini Ujerumani, zinaonesha ukosefu wa ajira unaongezeka nchini Kenya na utafikia asilimia 7.5 mwaka 2027 kutoka asilimia 6.3 hivi sasa.

Alisema pamoja na maandamano yale yaliyotokea siku chache zilizopita yaliyogeuka wakati fulani kuwa ya vurugu anaamini wananchi wanayo haki ya kueleza hisia zao kwa sababu Kenya ni taifa la kidemokrasia.

Sehemu ya vuguvugu la maandamano hayo yaliyosababisha vifo vya zaidi ya watu 20 kutokana na makabiliano kati ya waandamanaji na vikosi vya usalama ilikuwa ni shinikizo la kumtaka Ruto aondoke madarakani.

Shinikizo hilo halikufanikiwa lakini baadhi ya makundi ya vijana yaliapa Ruto atakuwa rais wa muhula mmoja na watahakikisha hatorejea madarakani 2027 muhula wake wa kwanza utakapomalizika.

Alipoulizwa kuhusu wasiwasi huo, Rais Ruto alisema „Sina wasiwasi wowote kwa sababu kufikia mwaka 2027 Wakenya watakuwa wameona matokeo ya mipango niliyo nayo."

**DW**



Maofisa wa Usalama wakiwa wanahakikisha hali ya ulinzi inaimarika baada ya kisa cha risasi karibu na uwanja wa gofu alikokuwa akicheza mgombea wa urais, Donald Trump, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Trump anusurika jaribio lingine la kuuawa

**WASHINGTON,** Marekani

MGOMBEA wa urais nchini Marekani kupitia Chama cha Republican, Donald Trump, amenusurika tena kwenye jaribio lingine la kuuawa, baada ya risasi kadhaa kufyatuliwa karibu na uwanja wake wa mpira gofu uliopo West Palm Beach, Florida.

Shirika la Ujasusi nchini humo (FBI), lilisema jana kuwa Trump, alilengwa katika kile walichotaja jaribio la kumuua, na kwamba idara ya usalama inachunguza tukio hilo lililotokea muda mfupi kabla ya saa nane za mchana wa juzi, kwa majira ya eneo hilo.

Ilielezwa kuwa risasi zilifyatuliwa kutoka nje ya uzio wa uwanja huo, huku maofisa wakisema uwanja huo ulifungwa ili kutoa fursa kwa Trump kucheza.

Baada ya muda maofisa hao wa usalama wa idara ya ulinzi wa wiongozi walimuona mtu akiwa na silaha aliyekuwa akichungulia kutokea nje ya uwanja huo kupitia matundu yaliyokuwa kwenye uzio wa uwanja na ambayo yanamwezesha kuona hadi ndani ya uwanja.

Gazeti la Washington Post la nchini Marekani, liliripoti kwamba Trump alikuwa akicheza gofu kwenye uwanja huo wakati kulipotokea tukio hilo na maofisa wa idara ya ulinzi wa viongozi walimkimbiza kwenye chumba maalumu cha mafichoni kilichoko kwenye uwanja huo.

**Gazeti la Washington Post la nchini Marekani, liliripoti kwamba Trump alikuwa akicheza gofu kwenye uwanja huo wakati kulipotokea tukio hilo na maofisa wa idara ya ulinzi wa viongozi walimkimbiza kwenye chumba maalumu cha mafichoni kilichoko kwenye uwanja huo.**

Ikulu ya White House ilisema kwenye taarifa yake kwamba Rais Joe Biden na Makamu wake, Harris wametaarifiwa juu ya tukio hilo na walipata ahueni baada ya kujua kwamba yuko salama.

Harris ambaye pia ni mgombea katika kinyang'anyiro cha urais nchini humo aliandika kwenye mtandao wa X kwamba uhalifu hauna nafasi yoyote nchini Marekani.

Mshirika wa karibu wa Trump, Lindsey Graham alisema amezungumza na Trump baada ya kisa hicho na amemwambia kwamba yuko salama na bado ni miongoni mwa watu wenye nguvu kabisa.

Mtoto wa Trump, Donald Trump Jr, alinukuu jeshi la polisi kwenye eneo hilo na kusema kupitia mtandao wa X kwamba, wamekuta bunduki aina ya AK-47, kwenye pori, kamera na begi la mgongoni na linaendelea kufanyia uchunguzi.

Taarifa zimesema, Trump alirejea nyumbani kwake Mar-a-Lago.

Aidha, siku chache zilizopita Trump alijeruhiwa kwa risasi sikioni, katika jaribio la kumuua la Julai 13 huko Pennsylvania na kuibua maswali kuhusiana na usalama wa wagombea urais, miezi kadhaa kabla ya kufanyika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Novemba 5, mwaka huu ambako atakabiliiana na Makamu wa Rais wa Chama cha Democratic, Kamala.

Ilielezwa kuwa kwenye tukio hilo, mtu mmoja aliyehudhuria mkutano wa hadhara ambako shambulizi lilitokea, aliuliwa kwa risasi. Ambaye alikuwa mshambuliaji, kijana wa miaka 20 Thomas Croocks, pia aliuliwa kwa risasi na Usalama wa Taifa.

Kaimu Mkurugenzi wa idara hiyo alisema Agosti kwamba alifedheheshwa na kitendo hicho kilichoonyesha udhaifu wa idara hiyo, uliotengeneza ombwe la jaribio hilo la mauaji. **DW**

## HABARI MICHEZO

# MFUNGAJI BORA WA ZANZIBAR AANZA KUWATISHA AZIZ KI, FEI TOTO LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI bora wa Ligi Kuu Zanzibar, Selemani Mwalimu, ameanza kuwa tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akipachika mabao matatu katika mechi nne ambazo ameichezea timu yake ya Fountain Gate, akikaa juu ya kilele cha orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Juzi kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, straika huyo alipachika bao moja, likiwa ni la tatu mfululizo kwake kwenye Ligi Kuu, akiisaidia timu yake kupata sare ya mabao 2-2 dhidi ya Dodoma Jiji FC.

"Nashukuru Mungu nimeanza vizuri Ligi ya Tanzania Bara, naamini nitafanya vema kama nilivyokuwa nikifanya Zanzibar, mimi kazi yangu ni kufunga, naomba tu nisipate majeraha, nitaendea kufunga," alisema mchezaji huyo aliyesajiliwa na Fountain Gate msimu huu akitokea KVZ ya Zanzibar.

**Akiwa na timu hiyo Zanzibar aliibuka mshindi wa kiatu cha dhahabu akimaliza akiwa na mabao 20, na ,asisti' saba, jambo ambalo liliwavutia mabosi wa Fountain Gate.**

Akiwa katika ligi mpya, hakufunga kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Simba, Agosti 25, mwaka huu, timu yake ilipochapwa mabao 4-0, Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam, lakini baada ya hapo alifunga bao moja kila mchezo.

Alifunga bao moja, Agosti 29, timu yake ikiichapa Namungo mabao 2-0, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, Lindi, akipachika lingine, Septemba 11, mwaka huu, na kuipa ushindi wa mabao 2-1 timu yake dhidi ya KenGold, kabla ya juzi kufanya tena hivyo dhidi ya Dodoma Jiji na kuipa sare timu yake inayoshika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba.

**KWISHINE!...**




Beki wa Arsenal, Gabriel Magalhaes (katikati), akishangilia sambamba na mlinzi mwenzake wa kati, William Saliba (kulia) na kiungo Thomas Partey, baada ya kuifungia timu yao bao pekee wakati ikishinda 1-0 dhidi ya Tottenham kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Tottenham Hotspur juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Black Sailor yapongezwa kuzindua jezi

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya Black Sailor FC imezindua jezi kwa ajili ya msimu huu mpya wa Ligi 2024-2025.

Timu hiyo ambayo inacheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, imezindua jezi tatu ambapo rangi nyeupe ni kwa ajili ya michezo ya nyumbani, machungwa kwa mechi za ugenini pamoja na jezi ya rangi ya ndimu ambayo ni ya akiba.

Hafla hiyo ilifanyika jana katika ukumbi wa ofisi ya timu hiyo huko Magomeni Jitini, visiwani hapa.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mgeni Rasmi, Dk. Khalid Bakari Amrani, ambaye ni Mratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dodoma, aliwapongeza kwa hatua kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha timu hiyo inakwenda kisasa zaidi.

Alisema hatua ya kuwa na jezi yako mwenyewe ya kuchezea ni jambo ambalo linafanywa na klabu zote duniani.

Amrani alisema hapo awali ilizoeleka kwa baadhi ya timu za Zanzibar kununua jezi za kawaida zinazouzwa katika maduka mbalimbali hapa nchini hivyo hatua iliyofikiwa na klabu hiyo kuzindua jezi zake itasaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza timu hiyo kupitia katika msimu huu wa ligi.

"Jezi hizi mbali na kuitangaza timu, lakini pia itakuja na mtindo wa biashara ambapo timu hiyo itanufaika," alisema.

Aidha, aliipongeza Kampuni ya Bima ya Amani Central Agency kwa kuwa wadhamini wakuu timu hiyo licha ya kutopata faida hasa kwa soka la Zanzibar.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mwenyekiti wa Black Sailor FC, Maulid Shaaban, alisema timu hiyo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuzalisha wachezaji ambao wanacheza madaraja mbalimbali katika Ligi za Zanzibar.

Alisema lengo la Black Sailor FC si tu kucheza Ligi Kuu au kuwa Bingwa wa Ligi ya Zanzibar, bali ni kuendelea kutoa wachezaji wazuri kupitia timu yake hiyo na zile za madaraja ya vijana.

Timu ya Black Sailor ilianzishwa mwaka 1981 katika maeneo ya Kidongo Chekundu visiwani hapa na imewahi kucheza hadi Ligi kuu Zanzibar katika misimu tofauti.

## Taasisi za serikali zatakiwa kufanya mabonanza

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za Serikali zimetakiwa kufanya mabonanza ya michezo hatua ambayo itasaidia kuimarisha afya za wafanyakazi, ili kuleta manufaa kwa taifa kwa kuongeza idadi ya wachezaji na wawakilishi katika mashindano ya kimataifa.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, kwenye bonanza la michezo la wafanyakazi lililoandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania, TBS.

Msigwa aliipongeza TBS kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuhamasisha michezo maeneo ya kazi kwa kutengeneza bajeti na kuruhusu wafanyakazi kushiriki michezo ili kuimarisha afya zao na kujenga mahusiano mazuri kazini, jambo ambalo alisema linaongeza ubunifu na ufanisi maeneo ya kazi.

Aliishauri Bodi na Menejimenti ya TBS kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga viwanja bora maeneo ya kazi ili kuwaweka wafanyakazi katika mazingira bora wakati wa kushiriki michezo mbalimbali.

Naye Mwenyekiti wa Bodi TBS, Prof. Othman Chande Othman, alisema walianzisha bonanza hilo miaka mitano iliyopita ambapo limelenga kuimarisha afya za wafanyakazi pamoja na kujenga umoja.

"Wachezaji wanacheza kama timu mbili tofauti, lakini ni walewale wakishamaliza mchezo wanaenda pamoja inaongeza urafiki," alisema Prof. Chande.

Aidha, Prof. Chande alisema mashindano hayo ya mabonanza yatachangia kuwa na machaguo mengi ya wachezaji watakaowakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa.

Naye Mwenyekiti wa Michezo wa TBS, Nyabutwenza Methusela, alisema bonanza hilo linasaidia watumishi kuondokana na changamoto ya afya ya akili kwa kujikita zaidi katika michezo ambayo inawaondolea msongo wa mawazo na kuongeza ufanisi wanaporudi kufanya kazi.

"Kupitia michezo afya ya akili na mwili inaboreshwa, wafanyakazi wanakuwa wachapakazi kwa sababu wameboresha afya zao za akili pamoja na mwili," alisema Nyabutwenza.

## ZISIKUPITE

### ANTHONY ASITA KUONDOKA

WINGA wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, anasita kuondoka Manchester United licha ya Fenerbahce kumtaka. (***ESPN***)

### TRIPPIER UTURUKI NDIO BASI

KLABU za Super Ligi za Uturuki Istanbul Basaksehir, Fenerbahce, Besiktas na Eyupspor, zimekata tamaa kujaribu kumsajili Kieran Trippier baada ya Newcastle United kuweka wazi kuwa wanataka kusalia na beki huyo wa zamani wa Uingereza mwenye umri wa miaka 33. (***Sky Sports***).

### VILLA NA DURAN

KLABU ya Aston Villa ilimthamini sana Jhon Duran hivi karibuni walikataa ofa ya puani milioni 40 kwa mshambuliaji huyo wa Colombia mwenye umri wa miaka 20, katika msimu wa majira ya joto. (***Mirror***)

### NEWCASTLE MAMBO SAFI

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe na Mkurugenzi wa Michezo, Paul Mitchell, wametatua tofauti zao na sasa wanaangazia uhamisho wa Januari, ikiwa ni pamoja na kumleta beki wa Crystal Palace ya England, Marc Guehi, 24. (***Telegraph***)

### SANCHEZ SASA AFUATILIWA

KLABU ya Manchester United inamfuatilia beki wa kulia wa Sevilla, Juanlu Sanchez, 21. (***AS***)

### CHELSEA UWANJA MPYA

CHELSEA imefanya mazungumzo kuhusu kuondoka Stamford Bridge na kujenga uwanja mpya katika eneo la Earl's Court. (***Guardian***)

### SPURS NA ROMERO

KLABU ya Tottenham Hotspur ilikataa ofa za kumnunua beki wa Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 26, wakati wa dirisha la uhamisho la majira ya joto. (***TyC Sports***)

### COOPER ANUKIA CSKA SOFIA

MLINZI wa Scotland, Liam Cooper mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kujiunga na CSKA Sofia kwa uhamisho wa bila malipo baada ya kuondoka Leeds United mwishoni mwa msimu uliopita. (***Football Insider***)

### EVERTON KUNUNULIWA

MFANYABIASHARA wa Marekani, John Textor ana imani kuwa dili la kuinunua Everton linaweza kukamilika baada ya wiki nne. (***Guardian***)

### MANGAN ATOSWA MADRID

ANDY Mangan wa Stockport County amezuiwa kujiunga na timu ya makocha ya Real Madrid baada ya kunyimwa kibali cha kufanya kazi kwa sababu ya kanuni za Brexit. (***Times***)

### CHUKWUEMEKA KWA MKOPO

KLABU ya Galatasaray ina nia ya kumsajili kwa mkopo winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20 kutoka England, Carney Chukwuemeka. (***Teamtalk***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AANIKA SPURS ILIVYOMNYIMA USINGIZI

**LONDON,** England

**●●● Sikufurahia maandalizi kwa sababu sikulala sana, niliposikia tumepoteza wachezaji...**

MIKEL Arteta amekiri matatizo ya upatikanaji wa kikosi Arsenal yalimfanya kukosa usingizi katika maandalizi ya mechi ya Jumapili ya London Kaskazini pale Tottenham, lakini akapongeza uthabiti wa timu yake walipopata ushindi muhimu wa bao 1-0.

**Bao la kichwa la Gabriel Magalhaes dakika ya 64, lilisuluhisha mechi kali kwa upande wa Arsenal, huku timu ya Arteta sasa ikiwa imeshinda mechi tatu mfululizo za ligi za ugenini huko Spurs kwa mara ya kwanza tangu 1988.**

Arsenal walikuwa bila Declan Rice kwa kufungiwa pamoja na majeruhi Martin Ødegaard, Mikel Merino na Riccardo Calafiori.

Ødegaard na Calafiori walipata majeraha wakiwa kwenye majukumu ya kimataifa huku Takehiro Tomiyasu na Kieran Tierney pia wakiondolewa.

"Sikufurahia maandalizi kwa sababu sikulala sana," alisema Arteta.

"Nilitayarisha mikutano yote, vipindi vya mazoezi na kila kitu. Kisha nikapata habari kwamba tumepoteza mchezaji, na kisha mchezaji mwingine na mchezaji mwingine, ikabidi nibadilishe kabisa na kurekebisha mpango kwa wachezaji, tulikuwa na fursa kwa hiyo, ilikuwa ni changamoto kubwa.

"Pili tulipoanza kupata habari hizo, timu ilizidi kuwa na njaa ya kucheza mchezo huo. Ni pongezi kubwa kwa kila mtu kwenye klabu kuwa na tabia fulani. Ni wiki ngumu inakuja na badala ya kutafuta visingizio vyovyote tulivyofanya, kinyume chake tulikabiliana na changamoto, tulicheza kwa ujasiri na kutambua sifa tulizokuwa nazo kushinda mchezo huo."

Ødegaard alipata tatizo la kifundo cha mguu ambapo daktari wa timu ya Norway, Ola Sand, alipendekeza kuwa atamtenga nahodha huyo wa Arsenal kwa muda wa wiki tatu, hivyo kumfanya akose safari ya Alhamisi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta na ziara ya Jumapili kwa mabingwa wa Ligi, Manchester City.

## HABARI MICHEZO





# RABIOT SASA MALI YA MARSEILLIE

**MARSEILLE,** Ufaransa

ADRIEN Rabiot amekubali kujiunga na miamba ya Ligue 1 Marseille, timu hiyo ya Ufaransa, imethibitisha.

Rabiot amekuwa mchezaji huru tangu mkataba wake na Juventus ulipomalizika msimu wa majira ya joto na hakuwa na haraka ya kukubaliana na uhamisho wake ujao, akiwa na furaha kusubiri hadi dirisha la uhamisho lifungwe ili kupata ofa bora zaidi.

Manchester United, ambao ni wapenzi wa muda mrefu wa Rabiot, walihusishwa kwa mara nyingine tena na kiungo huyo, lakini ni Marseille ambao wameshinda mbio za kuwania saini yake wakisubiri uchunguzi wa kimatibabu.

Kwa Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ni kurejea Ufaransa kwa mara ya kwanza tangu 2019, alipowaacha wapinzani wakali wa Marseille Paris Saint-Germain. Pande hizo mbili zitakutana katika ‚Le Classique‘, mojawapo ya mechi zinazotarajiwa kwa hamu kwenye kalenda ya Ufaransa, mwishoni mwa Oktoba.

Nia ya United kumsajili Rabiot msimu huu wa majira ya joto haiaminiki kuwa ilikuwa ya juu sana.

Waliikuwa wameifukuzia saini yake mnamo 2022 na 2023, hata walifanya mazungumzo na mama yake na wakala mwaka jana.

Veronique Rabiot alikanusha madai ya kutaka kuhamia Old Trafford kushindikana kwa sababu ya mahitaji yake ya kifedha katika mahojiano na La Gazzetta dello Sport mnamo 2023, wakati kiungo huyo hatimaye alikataa nafasi ya kuondoka Juventus kwa uhamisho wa bure ili kuongezwa kwa mkataba wa mwaka mmoja.

„United walitaka kukutana nami ili kuonesha nia yao kwa Adrien, lakini hatukuwahi kuzungumza kwa kina kuhusu pesa kwa sababu aliamua kusalia Turin haraka,“ Veronique alisema. „Hakukuwa na mazungumzo yoyote ya kweli, na tuko kwenye makubaliano mazuri na Manchester United.“

# Ratiba ngumu kumstaafisha Akanji mapema

**MANCHESTER,** England

BEKI wa Manchester City, Manuel Akanji, ametania kwamba anaweza kustaafu akiwa na umri wa miaka 30 kutokana na kuongezeka kwa idadi ya mechi katika kalenda ya soka.

Akanji mwenye umri wa miaka 29, tayari amecheza mechi saba kwa klabu na nchi kwa muhula huu.

Alicheza mchezo wake wa mwisho wa msimu uliopita Julai 6, wakati Uswisi ilipochapwa kwenye Euro 2024 na kisha kuanza mechi ya kwanza rasmi ya kampeni za 2024-25 nchini Uingereza kwenye Ngao ya Jamii, Agosti 10, mwaka huu.

Wiki ijayo City wataanza kampeni yao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopanuliwa, na ratiba nane za ligi kabla ya awamu ya mtoano kuanza.

Watamaliza msimu kwa kushindana katika Kombe la Klabu Bingwa Dunia yenye timu 32, fainali ambayo imepangwa kuchezwa Julai 13.



“Ni ngumu sana,“ alIsema Akanji.

“Hufikirii tu kuhusu msimu huu - lakini pia msimu ujao. Wacha tuseme tutashinda ligi au kombe, kisha twende fainali ya Kombe la Dunia la Klabu; Ngao ya Jamii ni wiki tatu baadaye. Kwa hivyo ni lini tutakuwa na likizo?

“Hakuna mapumziko wakati wa baridi, kwa hivyo ikiwa tuna bahati tunapata wiki mbili na kisha tunahitaji kurejea na msimu ujao. Kisha msimu ujao wa majira ya joto ni Kombe la Dunia. Hakuna mwisho.“

Akanji amecheza mechi 48 za klabu katika kila moja ya misimu yake miwili kamili akiwa City, na anajitayarisha kwa kazi kama hiyo msimu huu.

“Ni mchezo baada ya mchezo tu na sijui itakuwaje katika miaka michache ijayo,“ alingeza. „Huwezi kuendelea kuongeza mchezo baada ya mchezo na kudhani kila kitu kitakuwa kama ilivyokuwa. Lazima ufikirie kuhusu wachezaji pia.

“Wakati fulani utakuwa umechoka sana kucheza michezo yoyote zaidi. Na kisha kupata majeraha, bila shaka. Tunafanya mazoezi kwa bidii iwezekanavyo na tuko sawa -lakini lazima kuwe na kikomo. Labda nitastaafu nikiwa na miaka 30.“

## Yamal atabiriwa kuwa kama Messi

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Girona, Michel, amesema Lamine Yamal anaweza kufikia kiwango cha Lionel Messi baada ya kumtazama winga huyo wa Barcelona akitenganisha timu yake katika mchezo wa Jumapili wa dabi ya Katalunya.

Yamal mwenye umri wa miaka 17, alifunga mara mbili Barca iliposhinda mabao 4-1 na kuifanya kushinda mechi mara tano mfululizo kwenye LaLiga msimu huu, huku Dani Olmo na Pedri pia wakifunga pia, kabla ya Cristhian Stuani kuifungia Girona bao la dakika za lala salama.

"Lamine ni mleta tofauti,“ alisema Michel katika mkutano na wanahabari. „Kwangu mimi, tayari ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani akiwa na umri wa miaka 17.

"Ni vigumu kufikiria kwamba baada ya Messi angekuja mwingine kama yeye, lakini ninatumaini Lamine ataendelea kuimarika.“


Yamal alifunga mabao mawili katika dakika saba za kipindi cha kwanza na kuua mchezo kabla ya mapumziko.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania sasa anaongoza ligi kwa kuchangia mabao msimu huu akiwa nayo saba, mbele ya wachezaji wenzake Robert Lewandowski na Raphinha.

Kabla ya mechi ya Jumapili dhidi ya Girona, mabao manne kati ya matano ya Yamal yalikuwa yamefika kupitia pasi za mabao, huku Kocha wa Barca, Hansi Flick, akikaribisha kuongezwa kwa mabao zaidi kwenye mchezo wake.

"Nilifurahi sana kwa sababu alifunga bao,“ alisema Flick kuhusu majibu yake kwa bao la ufunguzi.

"Lamine kwa kawaida anatoa pasi ya mwisho na nilifurahi kwamba alifunga leo.“



## Fadlu aiona Simba tofauti kwa Mkapa

INATOKA UKURASA 24

zaji wa Simba uwanjani, huku kipa Aishi Manula akivamiwa na mmoja wa polisi aliyekuwa akiwalinda.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, alisema hali haikuwa shwari baada ya mchezo kumalizika kwani timu yao pamoja na waamuzi walifanyiwa vurugu.

"Baada ya mchezo kumalizika tulishauriwa na watu wa usalama kuwa tusitoke kule jukwaani tusubiri vurugu zipungue, wakati huo wachezaji wakaondoshwa uwanjani kwa pamoja kutoka katikati ya uwanja kwenda vyumbani huku wakirusha chupa.

Tulikaa vyumbani kama dakika 15 hivi, vurugu zikapungua, katika hali ya kushangaza, mtu ambaye alikuwa anatulinda ndiye aliyemvamia Manula tuliyekuwa tumekaa naye kule jukwaani na kumfanyia vurugu, lakini hajapata madhara yoyote.

"Tulikaa vyumbani na wachezaji kama dakika 40 kusubiri vurugu mitaani zipungue ndipo tulipoondoka," alisema Ahmed.

Alisema kufanya kwao fujo ni dalili za kukata tamaa kwani wanajua watapata shinda, Uwanja wa Benjamin Mkapa katika mchezo wa marudiano.

"Aina ya usajili walioufanya na walichokipata uwanjani hawakukitarajia, ni sare ambayo tuliitolea machozi, jasho na damu. Hili limekwisha akili yetu ni mechi ya marudiano," alisema.

## Gamondi avalia njuga janga la...

INATOKA UKURASA 24

na CBE Jumamosi kwenye mchezo wa marudiano, nahitaji tutumie nafasi kadri zinavyopatikana," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mchezo wa marudiano, alisema hautokuwa rahisi kama ambavyo wengi wanavyodhani, lakini akawataka mashabiki wa Yanga kufurika uwanjani kwani amewaandalia mambo mazuri.

Katika mchezo wa Jumamosi Yanga ilishinda bao 1-0, lililofungwa na straika raia wa Zimbabwe, ambaye amekuwa akilaumiwa kwa kukosa mabao mengi katika mchezo huo.

Yanga inahitaji ushindi au sare yoyote ili kuweza kutinga hatua ya makundi kwa mara ya pili mfululizo, ambapo msimu uliopita ilifanya hivyo na kuishia hatua ya robo fainali.

# NBC YASHIRIKI RUANGWA MARATHON, YAAHIDI MAKUBWA SEKTA MICHEZO

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeshiriki msimu wa pili wa mbio za Ruangwa Marathon 2024, huku ikisisitiza dhamira yake ya kuendelea kuunga mkono jitihada mbalimbali za wadau wa michezo nchini kupitia ushiriki, ufadhili, ubunifu na utoaji wa huduma mbalimbali zikiwamo za kifedha mahususi kwa wadau wa sekta hiyo.

Dhamira ya benki hiyo ni sehemu ya mkakati wake katika kuunga mkono jitihada za serikali na wadau hao katika kukuza vipaji, kujenga afya ya jamii na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana pamoja kusaidia ufanikishaji wa agenda mbalimbali za kijamii kupitia hamasa ya michezo.

Akizungumza wakati wa mbio hizo zilizofanyika katika Uwanja wa Madini wilayani Ruangwa mwishoni mwa wiki, zikiongozwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Meneja wa Kanda ya Pwani wa Benki ya NBC, Zubeider Haroun, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, alisema nia yao ni kuendelea kuwa mdau mkubwa wa sekta ya michezo nchini sambamba na kutumia vema huduma zake za kifedha katika kuwasaidia wadau wa sekta hiyo muhimu.

"Ushiriki wetu kwenye mbio hizi za Ruangwa Marathon ni wa namna mbili, kwanza tumeingia kama moja ya wadhamini muhimu wa mbio hizi na pia tumeungana na washiriki wengine akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pamoja na viongozi wengine wa serikali katika kukimbia mbio hizi sambamba na kushiriki matukio mengine yalioambatana na mbio hizi lengo likiwa ni kufanikisha agenda yake ambayo ni kuchochea maendeleo kupitia sekta ya afya, utalii na michezo," alisema.

Katika tukio hilo lililovutia washiriki takriban 5,000 wakiwamo viongozi wa serikali, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma, wasanii maarufu na wananchi ilishuhudiwa, Meneja huyo wa Kanda akiongoza maofisa wengine wa benki hiyo katika kushiriki mbio hizo akiwamo Meneja wa Tawi la Mtwara, Editha Mwakatobe na Meneja wa Tawi la Lindi, Iovin Mapunda.

"Tumekuwa tukizingatia sana agenda mbalimbali zinazoambatana na matukio haya ya kimichezo na hilo limekuwa likitupa msukumo mkubwa kushiriki, kufadhili na hata kuandaa matukio kama haya," alisema Zubeider huku akitolea mfano mbio za NBC Dodoma Marathon zinazoandaliwa na benki hiyo kila mwaka jijini Dodoma zikilenga kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Zaidi kupitia udhamini wake kwenye Ligi Kuu ya NBC (NBC Premier League), Ligi ya Vijana na Ligi ya Championship, benki hiyo pia imekuwa ikibuni na kutoa huduma mbalimbali za kifedha kwa wadau tofauti wa mchezo wa mpira wa miguu nchini ikiwamo mikopo ya usafiri kwa klabu na Bima ya Afya kwa wachezaji na mabenchi ya ufundi.

Akizungumza baada ya mbio hizo, Waziri Mkuu Majaliwa, pamoja na kuwashukuru wadau mbalimbali waliofanikisha mbio hizo ikiwamo NBC, pia alionesha kuridhishwa na mchango wa sekta ya michezo nchini katika kufanikisha jitihada mbalimbali zinazolenga kusaidia jamii ikiwamo afya.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati walioketi), akiwa pamoja na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi wa serikali, wasanii maarufu na wadhamini wa mbio za Ruangwa Marathon 2024 zilizofanyika mwishoni mwa wiki katika Uwanja wa Madini wilayani Ruangwa. Benki ya NBC ilikuwa moja ya wadhamini muhimu wa mbio hizo. **MPIGAPICHA WETU**

# BFT yalenga vipaji vipya Mara

**Na Shufaa Lyimo**

RAIS wa Shirikisho la Ngumi nchini (BFT), Lukelo Willilo, amefanya ziara ya kishindo Kanda ya Ziwa kwa kutembelea mikoa ya Mara na Mwanza, kuelekea mpango wao wa kuendesha mafunzo ya awali ya walimu, waamuzi, majaji na wasimamizi wa mchezo wa ngumi mkoani Mara baadaye mwaka huu.

BFT kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mara, wataendesha mafunzo ya awali ya walimu, waamuzi, majaji na wasimamizi wa mchezo wa ngumi katika mkoa huo Novemba mwaka huu, na kisha kuandaa mashindano ya Kumbukizi ya Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere, Aprili, mwakani.

Katika ziara hiyo ya rais huyo wa BFT iliyoanzia mjini Musoma, Mara akiambatana na Katibu Mkuu wa Shirikisho hilo, Makore Mashaga, walifanya mazungumzo na Serikali ya Mkoa wa Mara inayoongozwa na Mkuu wa Mkoa huo, Kanali Evans Mtambi.

"Mara ni mkoa wenye historia kubwa katika mchezo wa ngumi katika taifa letu, ikiwatoa wanamasumbwi bora na mahiri walioiletea sifa taifa letu kimataifa katika mchezo wa ngumi kwa nyakati tofauti," alisema Willilo na kuongeza;

"Mkoa wa Mara una hazina kubwa ya mabondia wenye kuweza kufanya vizuri kimataifa, wana faida za kibaiolojia, nguvu na ustahimilivu kama Shirikisho tumejipanga kuwekeza nguvu zaidi kuibua vipaji vipya vya vijana wadogo.

Michezo
Nipashe
Jumanne Septemba 17, 2024



Yamal atabiriwa kuwa kama Messi UKURASA 22

# FADLU AIONA SIMBA TOFAUTI KWA MKAPA

●●● Awaita mashabiki uwanjani kuwakabidhi jukumu la kuiua Al Ahli Tripoli Jumapili, asema...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema anaamini mashabiki wa timu hiyo watakuwa sehemu kubwa ya ushindi katika mchezo wa marudiano wa raundi ya kwanza, Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli ya Libya utakaochezwa Jumapili ijayo, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku akiamini itakuwa mechi tofauti kabisa na hiyo waliyocheza nchini Libya.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo wa mkondo wa kwanza juzi, Uwanja wa Juni 11, jijini Tripoli, Libya, Fadlu alisema umati wa mashabiki 45,000 uliokuwa ukihanikiza uwanjani hapo kwa kiasi fulani uliwaathiri wachezaji wake, lakini anaamini kuwa hata wao watapata faida hiyo watakaposhangiliwa na mashabiki kiasi cha 60,000, Uwanja wa Benjamin Mkapa, akisema hali inaweza kuwa zaidi na tofauti kabisa ya hicho walichokipata wao.

"Tunakwenda kuifanyia kazi mechi ya marudiano kwa kuendelea kuwasoma, leo wameweka baadhi ya wachezaji wapya ambao hatujawahi kuwaona na kuwafanyia kazi, lakini pia mashabiki wao na jinsi wanavyoshangilia ilitupa shida kidogo, ila najua nyumbani mashabiki wa Simba wanaweza kufanya zaidi yao katika mchezo ujao.

"Nawafahamu mashabiki wa Simba, wanaipenda timu yao na mara nyingi wapo nyuma ya wachezaji wao, najua watakuja wengi zaidi ya hawa, watawashangilia wachezaji wao, watawatoa mchezoni wapinzani zaidi ya walivyokuwa wanafanya hawa wa Al Ahli Tripoli, na matokeo yake tutapata matokeo mazuri," alisema kocha huyo raia wa Afrika Kusini.

Simba ililazimisha suluhu ugenini, matokeo ambayo yanaiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kama itapata ushindi wa aina yoyote.

Akizungumzia mchezo huo, aliwapongeza wachezaji wake, akisema wameonesha uwezo mkubwa wa kucheza wakiwa hawana mpira.

"Tulikuwa na kiwango kizuri, hasa kwa mabeki wetu na hata viungo, tumeonesha kuwa tunaweza kupambana kwa pamoja, tumeonesha jinsi gani tunaweza kucheza tukiwa hatuna mpira.

"Tulikosa nafasi moja kipindi cha kwanza, unajua mechi hizi nafasi zinapatikana kwa nadra sana, hivyo ilibidi zitumiwe," alisema.

Baada ya mchezo huo kumalizika vurugu kubwa zilitokea, ambapo mashabiki wa timu hiyo ambao walionekana kutoamini timu yao kama imeshindwa kupata ushindi nyumbani, hali iliyowalazimu watu wa usalama kuwaondoa haraka wache-

INAENDELEA UK. 23



Kiungo mkabaji wa Simba, Yusuph Kagoma, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Al Ahly Tripoli kwenye mechi ya mkondo wa kwanza Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Juni 11, jijini Tripoli, Libya juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: SIMBA**

## Gamondi avalia njuga janga la mabao Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kazi aliyokuwa nayo kuelekea mechi ijayo ya marudiano ya hatua ya kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia, ni tatizo la kukosa mabao linaloikabili timu yake kwa sasa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, kocha huyo alisema kuelekea mchezo ujao atalifanyia kazi tatizo hilo ili lisijirudie tena kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, Jumamosi ijayo.

Gamondi alitoa sababu ambazo anaamini huenda zilisababisha hilo, lakini hataki liendelee kwa vijana wake.

"Nahitaji kukaa nao na kuwaweka kwenye mtazamo na umakini ule ambao tumeuzoea, hii ya kukosa mabao nadhani imetokana na kutokuwa fiti pamoja na umakini. Sikuwa na wachezaji 14 ambao walikuwa kwenye vikosi vya timu za taifa, kitu ambacho kimesababisha wengi wasiwe kwenye viwango vya kawaida na umakini na hii huwa linatokea sana wachezaji wanapokwenda kwenye timu za taifa," alisema.

Alisema katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Abebe Bikila, Ethiopia, walikosa jumla ya mabao saba ambayo kama wangeshinda wangekuwa wamemaliza mechi ugenini.

"Sijafurahishwa na kiwango kwa sababu tumepoteza nafasi nyingi sana, tulikuwa tuimalize mechi kule kule kama tungepata nafasi zile kwa hiyo, ni lazima nilifanyie kazi kabla ya kukutana

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >